

**UHAKIKI WA USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA WALENISI
YA KATAMA MKANGI**

NA

ONG'ONDI, BOGONKO EVANS

**KUAFIKIANA NA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI
(MASTER OF ARTS)**

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2005


University of NAIROBI Library



0496773 3

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine



ONG'ONDI, BOGONKO EVANS
(MTAHINIWA)

Tasnifu hii imetolewa kutahiriwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii tuliotolewa na chuo kikuu hiki



DKT KINEENE WA MUTISO

NA



DKT OLALI, TOM

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa marhemu ndugu zangu: Patrick Ondieki, Simon Ochogo na dadangu Jane Nyasuguta. ambao waliniacha nilipowahitaji zaidi.
Mungu awaweke pema peponi!

SHUKRANI

Kwanza, namimina shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufikia hatua hii. Pia nawashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kuniwezesha kukamilisha kazi hii.

Nawashukuru wasimamizi wangu katika kazi hii: Dkt. Kineene wa Mutiso na Dkt. Olali Tom kwa mwelekeo na usimamizi wa kipekee pamoja na kunivumilia. Mungu awabariki. Pia ningependa kuwashukuru wahadhiri wengine katika Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kwa mafunzo na mawaidha yao. Hawa ni Dkt. Mwenda Mbatiah, Timothy Arege, Marehemu Richard Mgullu na Prof. Abdulalaziz.

Kadhalika nawashukuru wanafunzi wenzangu. Hawa ni: Kahiro Dancan, Japhet Mutua, Nicholas Otieno, Suzzy Nandama, Eunice Nangira, Jane Ochoki, Sarah Manzi na Vince Nyabunga. Tulishirikiana pamoja katika safari hii na nehema za Mwenyezi Mungu ziwe kwenu.

Sitasahau kumshukuru mke wangu Julie Kemunto na watoto wangu: Faith Kwamboka na Adams Ochogo ambao kwa sababu yao ninaishi na kung'ang'ana katika maisha. Wa mwisho na muhimu ni wazazi wangu kwa kunizaa na kunitunza. Pia na ndugu zangu wote kwa kunifaa nilipowahitaji. Kuna wengine ambao walinifaa na singeweza kuwataja kwa sababu ni wengi, kwenu nyote ninatoa shukurani zangu za dhati.

YALIYOMO	UKURASA
IKIRARI	i
TABARUKU	ii
SHUKRANI	iii
MUHTASARI	iv
SURA YA KWANZA	
1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo la Utafiti	4
1.2 Madhumuni ya Utafiti	6
1.3 Sababu za kuchagua somo hili	6
1.4 Mipaka Na upeo wa somo hili	7
1.5 Nadharia Tete	7
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili	8
1.7 Msingi wa kinadharia	9
1.8 Njia za utafiti	12
2.0 SURA YA PILI	13
3.0 SURA YA TATU	34
4.0 SURA YA NNE	55
5.0 SURA YA TANO	73
SURA YA SITA	
6.0 Hitimisho	86
6.1 Matokeo	88
6.2 Mapendkezo	89
MAREJELEO	90

MUHTASARI

Tasnifu hii imeshughulikia uhakiki na unakidi wa riwaya ya *Walenisi* iliyoandikwa na marehemu Mkangi na kutolewa kwa mara ya kwanza mwaka wa tisani na tano (1995)

Kazi hii tumeigawa katika sura sita. Katika sura ya kwanza, tumeweka wazi pendekezo la utafiti kwa kuonyesha tatizo la utafiti, sababu za utafiti wenyewe, nadharia tete, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti.

Vile vile tumeshughulikia upeo na mipaka ya utafiti huu miongoni mwa vipengee vingine vya pendekezo. Sura ya pili inahusu mtazamo kama kipengee mojawapo cha usimulizi. Katika sura hii tumejadili na kuweka wazi maana ya mtazamo na kuonyesha tofauti baina ya mtazamo na usimulizi.

Kadhalika, tumeshughulikia sawia mbalimbali za usimulizi katika riwaya ya *Walenisi*. Vile vile tumeonyesha aina za usimulizi na jinsi zinavyodhihirika katika riwaya hii.

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia unenaji na fikira kama kipengee cha usimulizi. Tumejadili aina tofauti tofauti za unenaji na fikira na kutoa mifano ya kudhihirika kwao katika riwaya hii.

Nayo sura ya nne, inaangazia wakati kama kipengee kimojawapo cha usimulizi. Katika sura hii, tumejadili maana ya wakati na umuhimu wake katika usimulizi. Pia tumeonyesha jinsi mbalimbali wakati hudhihirika katika hadithi.

Katika sura ya tano, tumejadili mpangilio na uwasilishaji kama kipengee cha usimulizi. Tumeonyesha wazi kuwa hadithi inaweza kuwa na mpangilio wa moja kwa moja au iwe na mpangilio changamano ambapo kuna uegemezaji. Katika riwaya hii kuna mtindo changamano ambapo tumeonyesha na kufafanua ni kwa nini Mkangi akatumia mtindo huu.

Vile vile, katika sura hii, tumeonyesha jinsi hadithi ya *Walenisi* imewasilishwa ambapo kuna mimesia na daigesia kama mbinu za uwasilishaji hadithi.

Tumehitisha katika sura ya sita kwa kurejelea tuliyojadili katika sura zote za awali kwa muhtasari tu. Kadhalika tumeelezea matokeo ya utafiti wetu pamoja na matatizo tuliyo kumbana nayo tukifanya utafiti huu. Hatimaye tumetoa mapendekezo kuhusu mtalaa huu.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Walenisi ni riwaya ya tatu ya Profesa George Katama Mkangi (1944–2004). Aliandika riwaya nyingine mbili: *Ukiwa* (1975) na *Mafuta* (1984). Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* zinafanana sio tu kimaudhui bali pia kimuundo. Kimaudhui riwaya zote zinaangazia matatizo ya kijamii na kiuchumi yanayokumba jamii za kifaraka huku akitoa mifano ainati ili kuonyesha kina cha athari ya matatizo hayo kwa jamii yenye matabaka.

Vilevile katika riwaya zote, ametuchorea jamii za kitabaka ambapo kuna tabaka la juu la matajiri na watawala kwa upande mmoja na la maskini kwa upande mwingine. Alisawin matabaka haya kiulinganuzi na kuonyesha sababu zilizobaini makundi hayo na hivyo kuonyesha mwanya bainifu kati yao.

Hadithi zinazopatikana katika riwaya hizi zimesimuliwa kwa muundo unaofanana ambapo kuna hadithi ya kimsingi inayoanza ambayo ina hadithi nyingine inayoegemezwa ndani yake. Katika *mafuta*, rafiki wawili wanafika mahali kuna muuza kunazi na wakiwa hapo kukatokea mtu anayejanbu kuiba kunazi ambaye anatoroka mbio anaposhutumwa kuwa mwizi na kuacha koti lililokuwa na makaratasi yaliyoandikwa hadithi ijulikanayo kama *Mafuta*. Marafiki hawa wanaanza kusoma hadithi hiyo ambayo inachukua nafasi kubwa ya riwaya yenyewe. Hadithi ya *Mafuta* ndiyo hadithi ya pili.

Hali inakuwa hivyo katika *Walenisi* ambapo Dzombo anahukumiwa kifo ambacho kinatekelezwa kwa sayari inayopaswa kumwagamizia mbali. Lakini kwa ujasiri anakiendesha chombo hicho na kutua katika nchi ya Walenisi. Hadithi egemezi katika riwaya hii ni changamano kwa jinsi inavyohusisha hadithi nyingi zilizounganishwa pamoja na zinazochunguza historia ya nchi ya Walenisi. Licha ya kufanana huku pia kuna tofauti katika usimulizi hasa tukizingatia jinsi mwandishi amefumbata vipengee mbali mbali vya usimulizi katika hadithi hii.

Ni muhimu kuelewa hadithi ni nini kabla ya kushughulikia uwasilishaji wake. Maelezo mbalimbali yametolewa kuhusu hadithi, na tunapochunguza baadhi ya maelezo

tunagundua kuwa dhana za wakati na mahali zimetiliwa mkazo Sababu ya mkazo huu ni kuwa matukio yanaposimuliwa huwa yanasimuliwa katika wakati fulani na mahali fulani. Kadhalika, matukio haya lazima yafuatane kimfululizo kulingana na kutokea kwao. Kwa mfano haitakuwa hadithi ikiwa mtu ameamka asubuhi akaenda kazini kabla ya staffahi kisha akarudi kustafahi kwa sababu matukio ya kuamka, kwenda kazini kisha kustafahi hayafuatani kiwakati Itakuwa hadithi ikiwa yamefuatana kiwakati jinsi yalivyotokea, yaani kuamka, kustafahi na baadaye kwenda kazini, chembilecho Barry (1995: 223):

“Hadithi ni masimulizi ya matukio yanavyotendeka kiwakati”

Tunapata mwengo wa maoni haya kwa Foster (1927:44) Hata hivyo ni muhimu kubaini tofauti kati ya hadithi na ploti kwa sababu katika hadithi kuna ploti Tofauti kati ya dhana hizi ni usababishi wa matukio, hivi kwamba matukio katika hadithi hayatokei hivyo bila sababu. Tunapobaini na kueleza sababu za kutokea kwa matukio, basi tutakuwa tunaieleza ploti ya hadithi hiyo kama anavyosema Foster(1927: 87):

“Ploti ni masimulizi ya matukio lakini mkazo unatiliwa kwa visababishi vya matukio hayo.”

Jambo jingine muhimu katika hadithi ni wahusika ambao Barry (1995) na Foster (1927) hawakuwataja katika maelezo yao Matukio katika hadithi hayawezi kutendeka pasipo na wahusika ambao hutenda, hutendewa na hutendeanana. Wanapotenda na kutendeanana, wahusika hupeleka hadithi mbele kiwakati na kipahala na hivyo haitoshi kusema kuwa hadithi ni masimulizi ya matuko kiwakati na kipahali bila kuwataja wahusika.

Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa hadithi ni masimulizi ya matukio yanayojengwa na matendo fulani ya wahusika, kulingana na jinsi yalivyotendeka kiwakati na kipahala Hata hivyo, swali ni je, matukio yafipofuatana, kiwakati na kipahala itakuwa hadithi au la? Jibu ni kuwa ni hadithi isipokuwa mwandishi ametumia mbinu ya kifasahi itwayo

mbinu rejeshi inayomwezesha kuvuruga mfuatano wa matukio kwa kuleta tukio la nyuma mbele na la mbele nyuma. Hali ikiwa hivyo kama anavyosema Wamitila (2002: 54):

*“Tumeweza kuchukua matukio yote na
kuyapanga jinsi yalivyotokea ili kupata mfuatano
wa matukio.”*

Kama hadithi inasimuliwa, basi swali la kujiuliza ni je usimulizi ni nini? Kabla la kujibu swali hili ni muhimu kuelewa unahusu nini usimulizi. Hadithi au simulizi inapowasilishwa huwa kumefumbatwa vipengee mbalimbali, ambavyo kwa ujumla vinachangia muundo wa hadithi, ambao unapochanganuliwa hupelekea kupata maana ya hadithi kwa jumla.

Kwa hivyo tunaposhughulikia jinsi vipengee anuwai vya usimulizi vinavyoleta maana huwa tunashughulika na usimulizi kama anavyoeleza Barry (1995: 222):

*“Usimulizi ni mtalaa wa jinsi simulizi
huleta maana.”*

Usimulizi una chimbuko lake katika fasihi simulizi ambayo ndiyo utanzu mkongwe zaidi wa fasihi, ambao kwao fasihi andishi ilibuka, chembilecho Said A. Mohamed (1995: 82):

*“Asili ya simulizi ni katika fasihi simulizi
ambapo msimulizi yupo mbele ya hadhira
hau ambayo inamwona, kumsikia na
hata kumgusa.”*

Tofauti ya kiusimulizi kati ya fasihi simulizi na andishi (riwaya) ni kuwa kuna msimulizi hai mbele ya hadhira hai katika fasihi simulizi kinyume na ilivyo katika riwaya (fasihi andishi) ambapo kulingana na Said A. Mohamed,

*"Kiwiliwili cha fanani hakipo tena, msimulizi
hai hayupo tena, vitendo vyake vya kushughulisha
hadhira katika majukwaa havipo tena." (83).*

Hali hii inamaanisha kuwa badala ya msimulizi hai, tunakuwa na sauti ya mwandishi ambaye haonekani na pengine hajulikani kwa sura. Hata kama hayupo (mwandishi) hutaka kuikora, kuipendeza, kuichekesha na hata kufanya hadhira yake ilie kimoyomoyo. Kwa ufupi mwandishi wa riwaya hutaka ashirikiane na hadhira yake ingawa mkabala wake hauwezi kudhihirika jinsi unavyodhihirika ana kwa ana katika fasihi simulizi. Genette asema (1972: 184):

*"Lazima katika maandishi (riwaya) zipatikane
mbimu nyingine, kwa sababu kiini cha usimulizi si
hadithi yenyewe bali ni jinsi hadithi
inavyowasilishwa."*

1.1 TATIZO LA UTAFITI

Katika utafiti wetu tutashughulikia riwaya ya *Walenisi*, iliyoandikwa na Mkangi. Tutaihakiki kwa kuzingatia kipengee cha usimulizi. Kama tulivyosema hapo awali usimulizi unarejelea jinsi hadithi inavyowasilishwa katika simulizi na hivyo inajikita katika kiwango cha dikosi, ambayo kulingana na Genette (1972: 93):

*"Ni ile hali ya kuendeleza hadithi katika
uwasilishi wa simulizi."*

Simulizi nayo kama wanavyosema Barthes (1975) na Chatman (1990); *"Ni chochote kinachosimulia hadithi"* Maelezo haya yanaamaanisha kuwa usimulizi unahusu aina zote za simulizi yaani za kifasihi na sizizo za kifasihi.

Asili ya usimulizi na simulizi ni katika fasihi simulizi kama ambavyo tumekwishataja, katika maandishi hasa ya riwaya, fanani na hadhira hai hawapo tena, badala yake kuna

sauti ya msimulizi inayotuongoza katika ulimwengu wa maandishi ya kubuni, ikitupitisha katika masafa na maeneo, nyakati mbalimbali, mawasiliano ya wahusika na utendano wao, tabia na sarkolojia zao.

Kwa hivyo tutaangalia vipengele mbalimbali vya usimulizi na ni jinsi gani Mkangi amefaulu au kutofaulu kufumbata vipengele hivyo katika uwasilishi wa hadithi katika riwaya yake.

Baadhi ya vipengele hivyo ni pamoja na vile Genette alivyojadili katika *Narrative Discourse* (1972). Na hivyo ni pamoja na mtindo wa usimulizi ambapo tutachambua mtindo na kuweka wazi na kubani kama ni wa kimimesia au wa kidaigesia Mtindo wa daigesia unajitokeza ikiwa msimulizi anaelezea tu matendo na usemi wa wahusika bila kuwaruhusu wazungumze

*"Mtindo wa daigesia haujumlishi maneno
ya wahusika yanavyopatikana katika
mazungumzo." (Wamitila uk 33).*

Kinyume cha daigesia ni mimesia ambapo simulizi inawasilishwa kwa kusawiri wahusika katika mandhari fulani wakizungumza, chembilecho Wamitila (2002: 126):

*"Katika nadharia ya na-ratolojia mimesia
hutumiwa kurejelea hali ya kuonyesha hadala
ya kusimulia."*

Kadhalika tutaangalia kipengee cha mtazamo na kuelezea kama hadithi imesimuliwa kwa mtazamo wa ndani au wa nje. Vile vile tutashughulikia fikira na unenaji na aina gani ya unenaji imetumika katika hadithi na ni kwa nini. Aidha tutachanganua ni jinsi gani wakati umeshughulikiwa katika hadithi na kubani kama matukio yamefuatana kiwakati au la

Mwisho kabisa tutaangalia mpangilio wa hadithi, na kwa kufanya hivyo tutaonyesha kama hadithi ina vihadithi vilivyoegemezwa kwa hadithi kuu na athari gani inayotokana na kuegemezwa huku.

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Lengo la utafiti huu ni kuhakiki riwaya ya *Walenisi* iliyoandikwa na Mkangi na kutolewa kwa mara ya kwanza 1995, kwa kuzingatia kipengele cha usimulizi

Tutachambua na kuweka wazi vipengele mbalimbali vya usimulizi na kutathimini ni vipi Mkangi alifumbata vipengele hivyo katika *Walenisi*. Kadhalika utafiti huu unanua kuonyesha ni vipi usimulizi unachangia uelewaji wa hadithi na muundo wake

1.3 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI

Uhakiki wa kazi ya kifasihi husaidia katika kuchanganua na kueleweka kwa kazi husika. *Walenisi* ni riwaya ambapo mwandishi ametumia mbinu ya kurefusha mandhari na kufumbata muktadha wa kihistoria ili kumulikia maswala mapana yanayohusu jamii yake na ulimwengu kwa jumla, na kwa njia hiyo kumhimiza msomaji kufungua macho kuyaangalia mazingira yake.

Kadhalika riwaya hii ina muundo usio wa kawaida, ambapo kuna hadithi kuu ambayo inahusisha hadithi nyingine ndani yake. Hadithi kuu inahusu maisha ya Dzombo katika nchi yake; ile ya pili inahusu maisha ya huko Walenisi alikofika baada ya kuhukumiwa kifo kwao.

Ni riwaya ambayo inamulika maisha ya jamii katika nyanja mbalimbali huku ikibanisha matatizo ya ukandamizaji na dhuluma na kusawiri picha ya jamii kielelezo.

Utafiti na uhakiki wa riwaya hii utatoa mchango mahususi kwa wasomi na hata waandishi wa riwaya kwa jinsi ambavyo tutashughulikia kipengee ambacho

hakijashughulikiwa na wahakiki waliotangulia kuhakiki nwaya hii. Kwa mfano Wamitla (2003), Mwita (2002), Aligula (2003) na Wasike (2003) wamechakiki nwaya hii lakini katika uhakiki wao, wameshughulikia dhamira, maudhui, wahusika na matumizi ya lugha.

Aidha wahakiki ambao wameshughulikia *Walenisi*, hawakufuata mikakati ya kitaaluma. Kwa mfano, hawakutumia nadharia yoyote katika uhakiki wao kama tunavyonua kufanya katika utafiti huu.

Vile vile tunaamini kuwa hakuna utafiti unaoweza kuchukuliwa kuwa umekamilika. Sababu yenyewe ni kwamba wahakiki hutofautiana kiitikadi na pia inategemea ni nini mhakiki fulani anataka kuhakiki. Uhakiki haushughulikiwi wakati mmoja tu ukaiisha kwani inategemea historia na mazingira ya kijamii. Katika kila kipindi cha historia, fasihi ya wakati uliopita yafaa kufasiriwa upya (Hough 1962:6).

Kwa hivyo, utafiti wetu utatoa mchango mahususi na kuwa nyongeza kwa yale ambayo tayari yamesemwa na wahakiki kuhusu nwaya hii.

1.4 MIPAKA NA UPEO WA SOMO HILI

Mbali na *Walenisi*, Mkangi aliandika nwaya nyingine mbili, lakini utafiti wetu utamulika *Walenisi* pekee. Wahakiki wanapochambua kazi ya fasihi aghalabu hushughulikia maudhui, dhamira, wahusika pamoja na lugha. Katika utafiti wetu hatutashughulikia mambo hayo yote, bali tutajifunga katika usimulizi wa hadithi ya *Walenisi* kwa kuchanganua vipengele mbalimbali vya usimulizi katika hadithi hii. Navyo ni pamoja na mtazamo, msimulizi wa hadithi, wakati na jinsi umeshughulikiwa, mpangilio wa hadithi na mbinu za unenaji na fikira.

1.5 NADHARIA TETE

Utafiti wetu utaongozwa na haiypothesisia zifuatazo:

- Usimulizi wa hadithi ya *Walenisi* umefumbata vipengee vyote vya usimulizi kwa minterafu ya Genette (1972).
- Muundo wa hadithi hii utaeleweka pindi vipengee hivi vitakapochanganuliwa.

1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Riwaya ya *Walenisi* imeshughulikiwa na wahakiki mbalimbali. Hata hivyo, tahakiki nyingi ambazo zinapatikana kuhusu riwaya hii ni miongozo ambayo inanua kuwasaidia walimu na wanafunzi wa shule za upili kuelewa kazi hii ambayo ni mojawapo ya riwaya zinazotahiniwa kwa hivi sasa. Iltahiniwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2000 na itatahiniwa mara ya mwisho 2005.

Kwa mfano, Wasike (2003) na Aligula (2003) wamehakiki riwaya hii kwa kuzingatia vipengee vya maudhui, wahusika na matumizi ya lugha. Kwa hivyo katika uhakiki wao hawakushughulikia kipengee cha usimulizi.

Wamitila (1988) katika *Unlocking Katana Mkangi's Walenisi: A case of parabolic narrative?* Katika Kiswahili juzuu 61 Dar es salaam. TUKI, anasema kuwa matukio mengi katika riwaya hii si ya kihalisia kwa vile kuna matumizi mapana ya mbazi, ngano, pamoja na hurafa, na hivyo anafafanua maana ya matumizi ya mbazi na hurafa na kuweka wazi hadithi kwa msomaji.

Waandishi wa kazi za fasihi hubuni lugha ambayo haisemi mambo waziwazi, yaani lugha yenye vitendawili ambavyo msomaji huitaji kuviagua ili aweze kuelewa kinachosemwa. Ni muhimu kuelewa kinachosemwa kabla ya kudadisi ni vipi kimesemwa. Hata hivyo, amepiga hatua kidogo, kwa kufafanua machache kuhusu usimulizi wa hadithi ambapo anasema:

“Riwaya ya walenisi imesimuliwa katika nafsi mbili kuu: nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Nafsi ya tatu imetambulishwa na viwakilishi vya nafsi ya tatu (a.....) Riwaya inapoanza inasimuliwa katika nafsi ya tatu. Hata hivyo kuma sehemu inayosimuliwa katika nafsi ya kwanza. Hii ni sehemu inayohusu matokeo ya utafiti wa Dzombo nchini Walenisi ” (uk 92).

Mawazo haya ni muhimu lakini hayatoshi kwa sababu yanahusu mtazamo na msimulizi wa hadithi. Ni muhimu kudokeza kuwa kuna vipengele anuwai vya usimulizi ambavyo wahakiki huyu hakuwifafanua kama tunavyonua kufanya katika utafiti wetu

Kadhalika amegusia viwango viwili ambavyo hadithi imesimuliwa. Kiwango cha kwanza kinahusu hadithi ya kimsingi na cha pili kinahusu hadithi ya pili ambayo imeegemezwa kwenye hiyo ya kimsingi. Mawazo haya ni mazuri lakini yanagefaa zaidi yanagechukuliwa kama kipengee kimojawapo cha usimulizi badala ya kuchukuliwa kama mtazamo. Sababu yenyewe ni kwamba maelezo hayo yanaeleza jinsi hadithi ilivyopangwa. (Barry 1995: 235).

Njogu na Chimerah (1999), wanafafanua usimulizi kama sauti ya uwasilishaji wa hadithi na hivyo kudai kuwa kuna aina mbili za usimulizi. Usimulizi wa mwandishi mwenyewe anapotumia nafsi ya tatu na usimulizi ambapo mmoja wa wahusika anasimulia hadithi. Mawazo haya ni muhimu kwa jinsi yanavyotuwezesha kujua ni nani anasimulia hadithi ambacho ni kipengee kimojawapo cha usimulizi na si usimulizi wenyewe. Labda ni muhimu kubainisha tofauti baina ya usimulizi na usimuliaji.

Usimulizi unahusu vile hadithi inavyowasilishwa na ni dhana dhahania. Usimuliaji, kwa upande wake, ni tukio la kusimulia hadithi na ni tukio la kiutendaji.

Kutobaini tofauti hiyo kumepelekea wengi wa wahakiki kuchukulia kuwa mtazamo na usimulizi ni sinonimu, jambo ambalo kwa hakika ni makosa ya kimsingi katika muktadha wa usimulizi.

Vile vile katika mtazamo, inafaa ieleweke ni katika mtazamo upi hadithi inasimuliwa mambo haya yote hayajabainishwa na wahakiki hawa na hivyo kuacha mwanya mpana sana unaonuliwa kuzibwa na matokeo ya utafiti wetu

1.7 MSINGI WA KINADIHARIA

Utafiti wetu utaelekezwa na nadharia ya naratolojia ambayo kama anavyosema Barry (1995: 222):

*“Ni nadharia ya miundo ya simulizi yaani
mtalaa wa jinsi simulizi hujenga maana
pamoja na hana na mbinu zinazotumika
katika usimuliaji hadithi”.*

Kilicho muhimu katika naratolojia si kusema na kufasiri hadithi bali ni kutalii muundo wa hadithi na ili kufanya hivyo, Todorov(1969: 106) anasema

*“tunahitajika kuchunguza sehemu mbalimbali
za muundo huo na kufafanua uhusiano uliopo
baina ya sehemu hizo”*

Fasili hii ya naratolojia inazua swali la ni nini maana ya simulizi. Wananadharia akiwemo Genette (1972) walipendelea maana finyu inayofunga simulizi kwa zile simulizi zilizosimuliwa kwa neno la mdomo. Wengine kama Barthes (1975), Chatman (1990) Pavel (1985), na Bal (85) wanasema: *“Simulizi ni chochote kinachosimulia hadithi”* na ni mtazamo huu tutakaotumia katika utafiti wetu.

Wananaratolojia hubainisha tofauti baina ya hadithi na ploti. Hadithi ni masimulizi ya matukio yanavyotendeka kiwakati, ilhali ploti ni matukio katika hadithi kulingana na yanavyotendeka huku mkazo ukitiliwa katika visababishi vyake na kuwasilishwa katika kile kinajulikana kama simulizi (Barry 1995: 223).

Tofauti hii ni muhimu kwa naratolojia ingawa wananaratolojia mbalimbali hutumia istilahi tofautitofauti kurejelea ploti na hadithi. Lodge katika *Working with Structuralism* anapendekeza istilahi za mwana-urasimi wa kirusi ambazo ni *fabula* badala ya hadithi na *Sjuzhet* badala ya ploti. Wahakiki wa kirusi walitazama mitindo ya kubuni hadithi ambayo hivi sasa watu wengine wanatumia Mtindo huo pia hujulika kama *Sujet* (Sjuzhet), yaani hadithi kama inavyosawiriwa na kuhaririwa na msimulizi wa hadithi

(ploti), tofauti na *fabula*, ambayo ni hadithi ilivyojengeka kwa kufuata matukio (kikronolojia)

Maandishi mengi ya kisasa kutoka Amerika ya kaskazini yanatumia hadithi lakini badala ya ploti, wanatumia diskosi. Mada ambayo yana mashiko kulingana na Barry (1995: 223):

*"sio suala la ploti linalohusika, bali pia kuna
mimbo, mtazamo, kasi na kadhalika, yaani
mpangilio wote unaoathiri simulizi."*

Historia fupi ya naratolojia inaweza kuhusishwa na Aristotle, Vladimir Propp na Gerald Genette. Aristotle katika andiko la *The poetics* anatambua mhusika na kitendo kama elementi muhimu katika hadithi na kusema kuwa tabia ya mhusika lazima ionyeshwe kupitia ploti. Hata hivyo, mawazo ya Aristotle yameegemea zaidi kwa yaliyomo (maudhui) na ploti kuliko usimulizi

Mwasisi mwingine wa nadharia hii ni Vladimir Propp ambaye alikuwa mwana – urasimi wa kirusi aliyehakiki miundo ya hurafa za kirusi na kuchapisha matokeo yake katika kitabu alichokiita *The Morphology of the Folktale*. Katika dibaji ya kitabu hiki anasema kuwa neno mofolojia lina maana ya mtalaa wa maumbo, na hivyo kitabu hicho kinahusu miundo na vijenzi vya ploti

Propp alichunguza hurafa 100 na kutambua matukio fulani yaliyozihusisha. Katika kazi hiyo anayarodhesha matukio hayo na viamili vyake katika mfuatano maalumu wa kiusababishi. Matukio aliyoyatambua yalikuwa 31

Mawazo ya Propp na Aristotle yalikuwa nguzo muhimu ya nadharia ya naratolojia. Kwa kutumia matukio 31 ya Propp kama vile; mtu mmoja kupotea kutoka kwa familia, nguli kukataliwa, nguli kutotii amn ya kukataliwa, adui wa nguli kupata habari kuhusu mhasinwa wake, mhasinwa kudanganywa, mhasiriwa kudanganyika na hivyo adui wake

kufaulu, adui kujeruhi mtu mmoja katika familia na kadhalika, tunaweza kuzalisha ploti ya hurafa yoyote ya kirusi sawa na vile tunavyozalisha sentensi mbalimbali katika lugha fulani (utendaji) ikiwa tumejiami na sarufi, sintaksia na msamiati (mfumo lugha) wa lugha hiyo.

Hata hivyo, mfumo wa Propp umeegemea sana kwenye ploti na kukosa kile tunachoweza kukita uwasilishaji wa simulizi, jambo ambalo limeshughulikiwa na Genette ambaye mawazo yake ndio tutakayotumia katika utafiti wetu. Kwa muhtasari huyu ameshughulikia mambo kama vile daigesia na mimesia katika hadithi, mtazamo, msimulizi wa hadithi, swala la wakati, mpangilio wa hadithi na usemi au uneni na fikira katika hadithi.

1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu utakuwa wa maktabani ambapo tutaanza kwa kuisoma riwaya ya *Walenisi* na kuelewa vema na kuichanganua. Pia tutasoma riwaya nyingine zilizoandikwa na marehemu Mkangi ambazo in *Ukiwa* (1975) na *Mafuta* (1984). Kusoma na kuzielewa riwaya hizi kutatusaidia kupata msingi mwema wa kuhakiki riwaya ya *Walenisi*. Kwa mfano kama mtindo wa uwasilishi katika hizo riwaya umefanana na wa hadithi ya *Walenisi*, na ikiwa ni tofauti tutabaini ni kwa nini.

Kadhalika tutasoma maandishi yoyote yanayohusiana na swali letu, makala na tasnifu mbalimbali kuhusu riwaya pia yatatusaidia kupata mtazamo mpana katika utafiti wetu.

Aidha tutasoma vitabu na maandishi mengine kuhusu nadharia ya naratolojia. Maandishi hayo yatatusaidia kuelewa nadharia hii na kuitumia vizuri.

Vile vile tutatafuta maoni ya wataalamu mbalimbali wa fasihi kuhusu mada yetu.

Mchanga wao utakuwa wenye manufaa kwetu.

SURA YA PILI

MTAZAMO NA USIMULIZI

Matukio yanapowasilishwa katika hadithi, huwa yanawasilishwa katika mshabaha fulani wa uono, yaani mtazamo fulani wa kuona vitu au matukio ya kibunilizi au kihistoria ili kutoa picha ya kweli kuhusu matukio hayo. Dhana ya mtazamo imewahi kufasliwa kwa njia mbalimbali, lakini fasili hizo zinaelekea kuwiana. Kwa mfano kulingana na kamusi ya *Oxford Advanced Learner (1948)*:

*"Mtazamo ni mwelekeo au maoni kuhusu
Jambo fulani"*

Wandishi hutumia mikabala tofauti kuonyesha nia au maoni yao kuhusu matukio na wahusika katika hadithi. Kamusi ya *Websters International* nayo inaeleza mtazamo kama *"Msimamo au hali fulani ambayo kwayo kitu huangaliwa na kuchanganuliwa"* (1750). Hii inamaanisha kuwa hadithi inavyosimuliwa, sauti inayotumiwa na mwandishi kusimulia hadithi aghalabu huchukua msimamo fulani kuhusu matukio katika ulimwengu wa hadithi.

Maelezo yanayasabihiana na hayo ni yale yalitolewa na Liberman (1968:92) kuwa:

*"Mtazamo ni msimamo wa kifalsafa wa
mwandishi pamoja na upendeleo wake wa
kijamii na kimawazo kuhusu matukio na wahusika
katika hadithi"*

Fasili hii ina mashiko kwa jinsi ambavyo inahusisha wahusika. Sababu yake ni kuwa wahusika ni kiambajengo muhimu katika hadithi kwa vile matukio ya hadithi yanatendwa na wahusika na yanahusu wahusika ambao wanaweza kuwa wameshinki katika hadithi hiyo au wanasimuliwa tu

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) inaelezea mtazamo kama

“Numna ya kuangalia au kutazama kitu au mtu.

Jinsi mtu anavyoangalia au kufikiria jambo.

Mawazo ya mtu juu ya jambo Fulani”

Kwa majibu wa maelezo haya, tunaweza kusema kuwa mwandishi anatumia nafsi tofauti na hivyo mitazamo mbalimbali kutoa maoni yake kuhusu wahusika na matukio yao hadithini. Tunapotathimini maelezo haya mbalimbali tunakuta kwamba yanalingana kwa sababu yanahusu msimamo, nia, maoni na upendeleo wa mwandishi kuhusu matukio na wahusika katika hadithi. Ni muhimu tukumbuke kuwa mwandishi siye msimulizi bali msimulizi ni sauti anayotumia mwandishi kusimulia hadithi, ambayo inaweza kuwa sauti ya mmoja wa wahusika au sauti ya wakala asiyejulikana kama tutakavyoona hivi punde.

Hata hivyo msimulizi anapotoa maoni yake, na kuelezea nia yake kuhusu jambo au tukio fulani, kimsingi huwa anaonyesha uhusiano wake na anachokizungumzia au anachokisimulia. Kwa hivyo maelezo ya Susan (1996:118) yanafaa zaidi kuhusu mtazamo. Yeye anasema:

“Mtazamo ni uhusiano kati ya uono na wakala anayeona na kinachosemwa au kinachoonwa. Uhusiano huu ni kiambajengo cha sehemu ya hadithi na yaliyomo katika simulizi”

Uhusiano huu ni muhimu kwa sababu kiini cha mtazamo ni vipi na ni kutoka wapi vitu vinaangaliwa na kuhukumiwa

Hata hivyo utambuzi na ufahamu wa matukio ni mfanyiko wa kisaikolojia unaotegemea msimamo wa anayeona. Kwa mfano, mtoto mdogo huona na kutambua vitu kwa njia tofauti na mtu mkubwa. Elementi za hadithi huwasilishwa kwa njia fulani ambapo tunakumbana na mtazamo wa hadithi. Je, mtazamo u vipi, na unatokea wapi? Haya ndio baadhi ya maswali tutakayojadili katika sura hii kwa mntarafu ya nwaya ya *Walenisi*.

Mtazamo unapokuwa wa msimulizi ambaye anashiriki katika hadithi kama mhusika, tunaweza kusema kuwa huo ni mtazamo wa ndani wa hadithi, yaani hadithi imewasilishwa kwa mtazamo wa ndani. Katika hali hii, sauti inayosimulia inatumia nafsi ya kwanza ambapo mhusika kama huyo anakuwa na nafuu kushinda wahusika wengine kwa jinsi ambavyo msomaji atamfuatilia kwa jicho la mhusika na kimsingi anaweza kukubaliana na mtazamo wake.

Mtazamo wa ndani unaweza kubadilika kutoka mhusika mmoja hadi mwingine, hali ambayo inatoa picha kamili kuhusu matukio ya hadithi kwa vile inaonyeshwa jinsi wahusika tofautitofauti wanavyoangalia na kuhukumu matukio na mawazo sawa kwa njia mbalimbali.

Tunapokuwa na sauti ya wakala asiyejulikana akiwasilisha matukio ya hadithi, tunasema kuwa hadithi imewasilishwa kwa kutumia mtazamo wa nje ambapo kiwakilishi 'a' cha nafsi ya tatu kinatumika. Kuna aina anuwai za mtazamo au usimulizi wa nafsi ya tatu. Kuna usimulizi maizi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi ana sifa za kiungu za kujua sin na ndoto za wahusika wote, anakuwa kila mahali kwa wakati mmoja na anajua tangu mwanzo hadi mwisho mambo yote katika hadithi, chembilecho Liberman (1968: 143):

"Msimulizi anajua kila kitu kinachohitajika kujulikana kuhusu wakala na mtukio, yu huru kwenda popote kila wakati anavyotaka kutoka kwa mhusika hadi mhusika na kusema anachotaka kuhusu unenaji na vitendo vya wahusika. Ana uwezo wa kujua ndoto hisia na nia za wahusika."

Pia, kuna usimulizi tunde unatumia nafsi ya tatu lakini unasimulia hisia, mawazo na mambo yanayojulikana na mhusika mmoja tu au wahusika wachache miongoni mwa waliomo katika hadithi. Kadhalika kuna usimulizi wa nafsi ya tatu unaojulikana kama horomo ambapo msimulizi anatoa habari tu na kuacha wahusika wa nwaya au hadithi wazungumze wenyewe bila yeye kuwaingilia katika yale wanayoyazungumza na kutoa ufafanuzi

Hatimaye kuna usimulizi penyezi wa nafsi ya tatu ambapo mara nyingi msimulizi hutoa mawazo yake kuhusu wahusika, matukio na dunia ya hadithi

Waandishi wengi wa nwaya aghalabu hutumia mbinu hizi zote za usimulizi katika nwaya moja na hivyo ndivyo Mkangi amefanya katika hadithi ya *Walenisi*. Mtazamo unatuwezesha kupata kiini cha hadithi na mshabaha wa uoni ambao kwao vitu vinaangaliwa na kuhukumiwa.

Hadithi ya *Walenisi* imefumbua mitazamo miwili tofauti, yaani imesimuliwa kwa nafsi mbili kuu Nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Sehemu ya hadithi inayosimuliwa katika nafsi ya kwanza inahusu matokeo ya utafiti wa Dzombo nchini Walenisi

Katika sura ya sita ukurasa 153, Dzombo anasimulia kwa nafsi ya kwanza (mtazamo wake) vile alihukumiwa kifo katika nchi yake kwa kupinga ubaradhuli na upopo na hivyo kutoa picha mwafaka kuwa katika nchi yake, watu hasa viongozi walifanya mambo kinyume na kawaida mithili ya popo anayejiniginisha kwa mti huku kichwa kikitangulia chini.

Baada ya utangulizi mfupi wa utafiti wake, Dzombo katika mtazamo wake, anatusimulia visa mbali mbali kuhusu kundi la watu wanaojulikana kama Wachuna. Kwa kufanya hivyo anaripoti kuhusu Wachuna na asili ya Uchuna kwa kutumia nafsi ya tatu hali ambayo inajulikana kama usimulizi wa homodigesia ambapo mhusika anasimulia simulizi ya kidigesia ambayo pia anahusika

Anasema kuwa Wachuna walikuwa watu wa kawaida, lakini baadaye walijiwa na hila ya kuwanyima wengine mahitaji muhimu yampasayo mtu kuwa nayo ili kuishi kama binadamu. Katika ukurasa wa 154, tunasoma,

~ *'Nani awezaye laushi bila chakula bora. nyumba,
afya bora na nguo bila ya uhohehahe*

na mataabisho mengi na magumu?

Visa vinavyoelezea jinsi Uchuna ulivyozuka ni hadithi au vihadithi egemezi na hivyo Dzombo anabadilisha kutoka nafsi ya kwanza na kuvinpoti visa hivyo kwa nafsi ya tatu Jambo hili ni muhimu kwa sababu usimulizi wa nafsi ya kwanza hauwezi kusawiri hisia fikira, saikolojia na hata ndoto za wahusika wengine. Hata hivyo, mtazamo ni wake (Dzombo) kwa sababu alitafiti mambo hayo kwa muda mrefu ili kufikia msimamo wake kuhusu Wachuna na asili ya uchuna.

Kisa cha kwanza ni kile cha moto ambapo mwindaji mmoja katika harakati za kuwinda anaamua kumtengeneza bibi yake ushanga. Alipokuwa akipekecha ili kutoboa mashimo cheche zinatokea na baadaye moto kulipuka na hata kumchoma kulungu ambaye tayari alikuwa amenaswa kwenye mtego. Mwindaji huyu anakataa kuwafichulia wenzake siri ya uvumbuzi huu na wanaotaka moto wanalazimika kumwendea naye anatoa masharti kuhakikisha kuwa anabakia kuwa mkintimba kigogo wa moto hali ambayo inazua uhusiano wa ubwana na utwana. Kisa hiki ni muhimu kwa jinsi ambavyo kinapanua ung'amuzi na ufahamu wa Dzombo kuhusu hali ya ubwana na utwana iliyokolea na kukita mizizi katika nchi alikotoka.

Kisa cha pili kinamhusu mchawi ambaye anavumbua dawa ya kutibu wagonjwa wa kuumwa na nyoka, baada ya kushuhudia vita vikali kati ya nyoka wawili, Bafe na Chatu. Chatu, baada ya kuumwa na kutapikiwa sumu na Bafe, anachimba mizizi na kubambua magome ya miti ili kujitibu. Kabla ya vita baina ya hawa nyoka wawili, watu wengi walikufa kutokana na kuumwa na nyoka. Lakini baada ya kushuhudia vita hivi, mchawi anavumbua dawa ya kutibu wagonjwa wa kuumwa na nyoka kwa kutumia mizizi na maganda. Baadaye alipanua utibabu wake kujumlisha aina zote za magonjwa. Watu wakampa vyakula ili asiende shambani na akajirundikia ziada na kuwa tajiri na kupata utukufu pamoja na familia yake.

Hatimaye kisa cha tatu kinahusu Wachuna wa ukoo wa Mabavu. Mabavu aliyekuwa shujaa wa kupambana na wanyama wakali, alimpenda msichana Kadzo lakini penzi la

Kadzo lilikuwa kwa Dutu aliyempa 'nyama ya ulimi. Ili kuhakikisha kuwa anapendwa na Kadzo, anafanya njama za kumteka Kadzo akisingizia kuwa ni simba na kwenda kumficha mbali ponna. Mabavu aliambiwa kuwa akimwokoza Kadzo akiwa hai ataozwa awe mke wake. Anafanya hivyo na kumwua simba kusingizia kuwa ndiye aliyemchukua Kadzo Hatimaye anamwoa Kadzo na kuendelea kutumia ujanja huu mara kadha kujipatia wasichana warembo

Mwishowe akawa anachukua tu wasichana na kuwabikiri ili wazazi wao wapate ulinzi wake na anaishia kutunga sheria za kikatili na kudumisha uhusiano wa kitabaka.

Visa hivi ni muhimu kwa jinsi ambavyo vinatupa historia ya Uchuna kuwa asili ya Uchuna ni ubinafsi uliopatikana kwa watu wachache waliotaka kujinufaisha ilhali wengine wakiteseka. Kadhalika, kwa kubadilisha kutoka usimulizi wa nafsi ya kwanza (mtazamo wa ndani) hadi nafsi ya tatu (mtazamo wa nje), Mkangi anafaulu kutanguliza matumizi ya fasihi simulizi. Kwa mfano kisa cha moto ni kisasili kinachoelezea jinzi moto ulivyovumbuliwa na kiza cha Mabavu ni mfano wa kisakale au mighani.

Kama tulivyodokeza hapo awali, visa hivi ni hadithi egemezi na hivyo Dzombo ni msimulizi wa kihomodigesia anapotumia nafsi ya tatu kusimulia hadithi ya kihomodigesia ambapo yeye mwenyewe ni mhusika. Visa hivi (kulingana na Dzombo) vinatusaidia kuelewa jamii ya sasa ya Walenisi na jamii atokako Dzombo Kadhalika hadithi ya egemezi (visa vitatu) inatusaidia kuelewa hadithi kuu ambapo inabainika kuwa Wachuna walijiendeleza kwa kulaghai wengine na kudumisha umwinyi, ukoloni na udhalimu.

Kulingana na mtazamo wa Dzombo Wachuna walijiimansa kwa kukintimbi nyenzo kuu za uzalishaji mali kama ardhi ambayo walijigawia wao kwa wao. Katika ukurasa wa 170, tunasoma,

*"Walihanithi na kuufanya udongo chombo
cha biashara na kamari. Tokeo lake
likawa wengi wakakosa hata pa kuzaliwa
ama pa kujenga – sahai pa kulima ili mtu
angalau ajipatie riziki yake "*

Baada ya kuwanyima mafalaha ardhi, Dzombo anatarifu kuwa walishindwa kulima na badala yake walitumia mabavu na kuwashurutisha wakulima kulima na kisha kuwapokonya mazao na kujita wakulima halisi.

Ili kuendeleza mfumo huu, Dzombo anatarueza kuwa viongozi walianza kutumia nguvu na kuanzisha magereza na kufanya jamii kuwa jamii ya kigereza iliyoongozwa kwa kutawaliwa na hofu na vitisho hivi kwamba hakuna tofauti kati ya kuwa gerezani au nje ya gereza. Hali hii ilikuwa kawaida katika jamii ya Dzombo ndipo alihukumiwa kifo kwa kupinga hali hiyo.

Hata hivyo, Dzombo anafanua kuwa matokeo ya kuwepo kwa mfumo huu wa utabaka katika jamii ni ukosefu wa huduma za kimsingi kwa wengi. Kwa kutumia kisa cha mapacha, Dzombo anatuonyesha tofauti katika jamii na jinsi maisha ya ndugu yanavyoweza kubaidika na hivyo kuonyesha athari kubwa ya tofauti za kitabaka zinazopaliliwa na mfumo wa kibepan unaofafanya watu kuwa wanyama.

Katika kisa hiki Metabu, mwanawe Medze anafaniki kutokana na ukosefu wa mahitaji ya kimsingi na huduma ifaayo ya afya. Kwa upande mwingine, mwanawe Chiheny (Mefuraha) anapata huduma nzuri bila kuteseka. Daktari anayemtazama mtoto wa Medze hana huruma, kudhihirisha ukweli kuwa ubebani umegeuzwa watu na kuwajaza unyama na wanaotiliwa maanani ni wenye uwezo.

Katika pekuapekua zake Dzombo anatambua na kutuambia kwamba, Wachuna walianzisha 'Fyanduzi' (aina ya serikali) ili kulazimisha umma kuti utawala wa kichuna kwa kutumia vyombo vya dola kama vile polisi. Katika ukurasa wa 188, Dzombo anasema:

*"Pia waliunda vikosi vya kila aina kutoka vya kitaifa
mpaka vya kibindi vyote hivi vikiwa ni silaha zao,
za kutisha, vilionyeshwa umma kwa maksudi,
kwenye maandamano ya kusherehekea utawala wao."*

*Wenyeji wenyewe hawakukosa kupata ujumbe huo.
Ujumbe wenyewe wakaubatiza "H.F.F.U." Yaani
"Hebu fanya fujo uone."*

Uchuna ulipoendelea kukatokea falme mbalimbali za Wachuna, ambapo Dzombo anatarifu kuhusu madola manne yaliyopimana nguvu. Dola ya Mashanki, ya Magharibi, ya Kusini na ya Kaskazini. Kila dola likijanbu kujipanua kushinda mengine. Wakati huu, mila, desturi, utamaduni na lugha za watawala ndizo zilifambulika na hivyo watawaliwa walianza kuwaiga watawala kwa kila njia sawa na vile nchi zilizokuwa na nguvu hasa kipindi cha ukoloni zilivyong'ang'ania makoloni na kuishia kulazimisha utamaduni, utawala na lugha zao kwa wenyeji wa makoloni.

Kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya tatu, Dzombo anajiweka katika hali nzun (nafuu) na yenye mamlaka zaidi kutuonyesha kwa mtazamo wake vipi uchuna katika kilele chake ulikiuka haki na mahitaji ya kimsingi kwa binadamu. Wachuna walisema,

*"Si lazima kila mtu ale ashibe, kula kwategemea
bahati ya mtu. Kazi ni bahati nasibu wala
si ya kuadhimisha ubinadamu. Matibabu
hayawezekani kwa kila mtu. itategemea
uwezo wa kifedha wa mtu binafsi, nyumba
si kwa wote hali kwa wale wana bahati
kuzinunua; si lazima mtu ajivishe, kuwa
uchi ni kimaumbile na si lazima
kila mtoto aelimishwe." (172)*

Dzombo anaeleza kuwa Wachuna waliweza kueneza uchuna baada ya kumiliki matambo ya uchawi, moto, na mabavu na kuyaunganisha kuunda Fyanduzi. Tambo la uchawi lilihusika na uganga, dini na sayansi. Tambo la moto lilihusika na ufundi uhandisi na teknolojia na tambo la mabavu lilishughulikia uwezo, nguvu, vyeo na mamlaka. Aidha utawala wao ulikita nyoyoni na akilini mwa waja wao walipotumia mafiga ya ulafi,

ujinga na uongo

Hata hivyo, Dzombo anatumia nafsi ya tatu kuakisi msimamo wake na kueleza kuwa kuwa hali hii haikudumu milele kwa sababu watawaliwa walirevuka na kuona unyama waliokuwa wakitendewa. Katika ukurasa wa 193-194, Dzombo anasema:

"Lakini haya yalikuwa ni mapambazuko, kwani uzuri wa mapambazuko ni kwamba hayazuiliki! Kwani kwa pole pole na kwa utaratibu, miale hii iliwaamsha wa kwanza wa pili wa kumi..... wa mia wa elfu ... wa mamia elfu... wa laki moja... wa milioni.... Wa mamilioni.... mpaka wa mwisho, ulimwengu wao wote ukawa macho "

Walipotanabahi, Dzombo anaeleza kuwa waliweza kuona unyama na uchafu uliokuwa kati yao, unyama wa wachache kushiba na wengi kufa njaa, unyama wa wachache kutawala wengi kwa mabavu, unyama wa kunyanyaswa na unyama wa dhuluma na wa kila ana.

Kwa hivyo, Dzombo anatoa picha ya kuaminika kuhusu historia ya Walenisi kwa kubadili mtazamo kutoka nafsi ya kwanza hadi mtazamo wa nafsi ya tatu ili kujiweka katika hali nzuri ya kuwafuata wahusika wote wa jamii ya Wachuna kupitia utafiti wa muda mrefu maktabani. Anatuamini kuwa utawala wa Wachuna uliwakandamiza watu na kuwanyonya. Kadhalika anatumia historia ya unyonyaji, mfumo wa umwinyi na ubepani na jinsi mfumo hiyo ilivyowatoa watu utu na kuwafanya wanyama kiasi kuwa viongozi wakawa wadhalimu na kutumia mamlaka vibaya na kuvuja mali ya umma hadi huduma za kimsingi kukosekana.

Kupitia Dzombo, Mkangi anafumbata ile mbinu ya kisanaa ya kurefusha masafa ya kiwakati na kimandhari na kufanya hadithi ionekane kuwa inasimulia matukio yaliyotendeka mbali na zamani sana, na ndio sababu mojawapo ya kubadili mtazamo hadi nafsi ya tatu. Baada ya kupoti matukio ya utafiti wake, Dzombo anamalizia kwa

kujitaja na hivyo kutukumbusha kuwa ni yeye mwenyewe aliyekuwa anatoa taanfa ya utafiti wake. Katika ukurasa 196, Dzombo anasema:

*"Nikiwa sasa nina fahamu si haba, ninajiandaa kuutali
vilivyo ulimwengu huu ili nizidi kujifahamisha juu ya
mapana na anarufu yake... Ni mimi, Mtu-Dzombo
wa BeDzombo. Hivi leo tarehe ya juhudi.
Juma la mwangaza. Mwezi wa fahamu
Mwaka wa usawa WAI.ENISI"*

Baada ya kuitalii sauti ya nafsi ya kwanza iliyotumiwa na Dzombo na jinsi ilivyobadilika kuwa nafsi ya tatu na ni kwa nini, inahalisi pia kutali usimulizi wa nafsi ya tatu katika hadithi hii.

Ni muhimu kudokeza kuwa nafsi ya tatu inaweza kuangaliwa kwa njia nne kwa mujibu wa hadithi ya Walenisi. Kwanza, kuna usimulizi maizi ambapo msimulizi anazijua sin zote za wahusika wote, na anaweza kuwa kila mahali kwa wakati mmoja, na anayejua tangu mwanzo mambo yote katika hadithi. Mtindo huu ndio umetumika sana katika hadithi ya Walenisi kama tutakavyoona hivi punde.

Pili, kuna usimulizi tinde wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi anaeleza hisi, mawazo na mambo yanayojulikana na mhusika mmoja au wachache tu miongoni mwa waliomo katika hadithi.

Tatu, kuna usimulizi horomo wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi hutoa habari tu na kuacha wahusika wa hadithi wazungumze wenyewe bila yeye kuwaingilia na kutoa ufafanuzi au maoni yake. Hatimaye kuna usimulizi penyezi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi, mara nyingi hutoa mawazo yake kuhusu wahusika, matukio na hata ulimwengu wa hadithi kwa jumla.

Tunavyojua ni kuwa, katika bunilizi au uhalisia, usimulizi ama wa nafsi ya tatu au ya kwanza unaweza kuripoti matukio katika hadithi kwa kutumia mtazamo wa mwingine.

Hivi ndivyo hadithi ya Walenisi inavyoanza, ambapo kuna sauti ya wakala asiyejulikana na aliye nje ya hadithi, anatoa kauli ya kwanza kwa kutumia mtazamo wa Dzombo mwenyewe. Katika ukurasa wa 1, msimulizi anasema:

"Dzombo hakutazamia huruma yoyote kutoka kwa hakimu"

Dondoo hilo hapo juu limetolewa katika mtazamo wa Dzombo hata ingawa siye anayesimulia kwa sauti yake. Hali hii inawezekana katika usimulizi maizi wa nafsi ya tatu kwa sababu msimulizi wa aina hii ana sifa ya kiungu za kuweza kujua fikira na sarkolojia za wahusika.

Kwa kutumia mbinu ya ulinganuzi na usimulizi wa nafsi ya tatu mwandishi anafaulu kututolea maelezo ya hali ilivyokuwa duniani (nchi atokayo Dzombo) na Walenisi.

Katika sura ya kwanza, Mkangi kwa kutumia usimulizi maizi wa nafsi ya tatu, anafaulu picha ya jinsi utawala wa nchi ya Dzombo ulivyokuwa ambapo vyombo vyote vya kudumisha haki vilikuwa miliki ya tabaka tawala. Katika ukurasa wa 1, msimulizi anasema:

*"Zama hizo, mahakama hazikuwa zikifuata sheria
kwa mjibu wa kulinda, au kutetea, wala kulinda
haki za binadamu kazi yake kubwa ilikuwa ni kumtia
huttani jeyote aliyepatwa na kisirani cha kushtakiwa"*

Mnyongaji halali amesawiriwa akifuraha kazi yake ya kunyonga kwa sayari, na kutokana na maelezo yake kuhusu serikali (utawala), tunapata kinaya, kwamba, nchi hiyo imetoka ushenzini kwa kutoua kikatili kabla ya kumfundisha aliyehukumiwa jinsi ya kukirubani chombo (sayari) cha kifo.

Tunasimuliwa jinsi utawala wa kimabavu unavyodumisha utengano baina ya watu pamoja na hisia za woga na ubinaji. Sababu yenyewe ni kuwa kuna baadhi ya watu wanaomwona Dzombo kama aliyejichongea, na hapo ndipo mwandishi anabadili mtazamo kutoka usimulizi maizi hadi usimulizi horomo wa nafsi ya tatu na hivyo

kuwapa nafasi wahusika wengine kuzungumzia yaliyomsibu, Dzombo kwa kutumia nafsi ya tatu ambapo kutokana na mazungumzo yao, wanajiona kama wenye bahati ambayo Dzombo hakuwa nayo

Suala la kabadili mtazamo katika usimulizi ni muhimu kwa vile linafanikisha uwiano katika usimulizi. Sababu yenyewe ni kwamba, matukio fulani yanasimuliwa vema katika mtazamo fulani. Hata hivyo, usimulizi uliotawala ni ule wa aina ya maizi ambapo, msimulizi yu nje ya hadithi na kuwafuata wahusika na kunpoti matukio yao popote waendapo na vile vile kuelezea hisia, saikolojia na ndoto zao.

Dzombo, baada ya kuhukumiwa kifo, na kuingizwa kwenye, chombo (sayari) ambacho kinapaswa kumwagamiza, tunaambiwa kuwa alitumia ujasiri mkubwa na kukwepa vizuizi vilivyokuwa njiani na hatimaye kutua katika nchi ya Walenisi, kwa usimulizi wa nafsi ya tatu (maizi), unaoakisita mtazamo wa nje tunaelezewa hatua kwa hatua yaliyomkumba Dzombo katika safari hii ya ajabu

Kama tulivyodokeza hapo awali, kuwa mtazamo ni uhusiano kati ya wakala anayesimulia na kunachosimuliwa na anayeona kisimuliwacho, tunaweza kusema kuwa, Dzombo anaepushwa na kifo, ili kufanikisha mabadiliko na kujenga jamii mpya

Yanayomkumba, katika safani kabla ya kutua katika nchi ya Walenisi ni mengi, kwa mfano anakumbana na majabali mbalimbali yakiwemo ya ujinga, magonjwa na udhalimu. Majabali haya ni istiani ya matatizo yanayokumba nchi zinaoendelea na ugumu ulioko katika kupata maendeleo (Yanayoashiriwa na safani yenyewe) katika nchi hizi.

Baada ya kunusuka kifo, Dzombo anatua katika nchi ya Walenisi na kulakiwa na jamii ya watu sita. Msimulizi anatarifu kuwa nchi hii (Walenisi) ni tofauti kimaendeleo na atokako Dzombo. Ili kuelewa chanzo cha tofauti hii wenyeji wake wanaandaa safani ya utu. Wakiwa safanni wanakumbana na hali tofauti ambapo Dzombo anapendelewa zaidi kuliko wenzake, jambo ambalo Dzombo analifasin kiduniani kuwa alikuwa na 'bahati' kuliko wengine.

Kadhalika mtazamo wa Dzombo kwa wanawake ni ule tu wa Duniani atokako. Haya yanajitokeza katika safari ya kupima utu wake. Katika ukurasa wa 57 anasema:

" Na kumbe hawa wanawake wa huku ni kama wa kwetu- ya kuhakisha kuwa wanaume wameshiba kwanza kabla ya wao wenyewe! Bahati gani hii Dzombo? "

Safari hii ya utu, ni hatua muhimu kwa kuonyesha kuwa kufikia afanifu katika jamii ni safari ngumu na ndefu inayohitaji juhudi ya kujitolea kwa hali na mali miongoni mwa wanajamii.

Vile vile, mwandishi anatumia usimulizi maizi wa nafsi ya tatu kufumbata mambo tofautitofauti yaliyoilemaza jamii ya Dzombo kama vile ufiada kwa kutumia kisa cha mzee Matigasi. Kisa hiki, sio kwamba ni Dzombo anayekisimulia kwa nafsi yake, badala yake msimulizi wa sifa za kiungu anapenya hadi akilini mwa Dzombo na kutuonyesha kuwa mzee Matigasi anatoa rushwa ili biashara yake iendelee kwa kuwa hana leseni (uk 91). Kwa hivyo wakala huyu wa nafsi ya tatu (maizi) aliye nje ya hadithi anatuonyesha kuwa jamii ya Wachuna na ile ya Dzombo ina mifumo ya kisiasa, kuchumi na kijamii yenye misingi ya ufiada inayofaidi tabaka la matajiri.

Kama tulivyotaja hapo awali, msimulizi aliye nje ya hadithi yuko katika hali nafuu ya kunpoti matukio ya ulimwengu wa hadithi kwa sauti yenye mamlaka zaidi ambayo inatunifu matukio mbalimbali katika hadithi ya Walenisi. Kwa mfano katika sura ya tano, Dzombo anaajabia anayovaona katika nchi ya ajabu- yaani maendeleo ya juu pamoja na muumano wa kijamii unaomfanya kupachukulia mahali hapo kuwa ahera, mambo ambayo yanajenga maudhui ya elimu na maendeleo katika riwaya hii. Mwandishi anaonyesha umuhimu wa elimu na utambuzi kwa kusawiri nchi mbili tofauti ambapo jamii atokako Dzombo haithamini elimu na hivyo inatawaliwa na ujinga, na ile jamii kielelezo (walehisi) inayothamini elimu na maendeleo kwa ujumla.

Matukio mengine ambayo yanaanfiwa kwetu ni yale ya ukatili na ubaguzi ambayo

yamefumbatwa katika jabali la udhalimu na maelezo mengine katika hadithi. Katika jabali la udhalimu tunasikia sauti mbalimbali zikipambana na hivyo kutuanfu kuwa ulimwengu unakumbana na ubaguzi wa kila aina. Kwa mfano kuna ubaguzi wa kijinsia ambapo mwanamke anadhulumwa uk 30-1, pia katika uk 135, tunasoma

*"Kwenu mwanamke ni embe, lililoiva, ukishalila huwa ni kokwe
(Kokwa) ya (la) kutupiliwa mbali .. kwenu mwanamke ni ndizi,
ukishalila huwa ni ganda la kutupiliwa (kutipwa) jaani..."*

Kadhalika kuna ubaguzi wa kidini baina ya Mkristo na Muislamu, Mwafrika mpagani na Myahudi Mlaghai, ubaguzi wa kimadhehebu kati ya Mprotestantu na mkatoliki na aina nyingine nyingi za ubaguzi kama vile wa kiuchumi, kikabila, wa rangi na kadhalika

Matukio haya yote yanaonyesha mambo ambayo, yanapelekea au yanachangia maudhui muhimu katika riwaya hii ambayo ni maudhi ya ukombozi. Visa vya ukatili, unyanyaswaji, udhalimu, matumizi mabaya ya mamlaka, na unyonyaji ndivyo vinavyochangia tabia ya Dzombo kama mwanaharakati na mwanamkombozi.

Sauti ya usimulizi, inayofumbata mtazamo wa nje inatuarifu kuwa, harakati zake za kukomboa jamii zinagonga mwamba kwanza kwa sababu tabaka tawala lilikuwa linamiliki vyombo madhubuti vya ukandamizaji kama polisi na mahakama Pili, wanajamii walikuwa wamekolezwa kasumba ya kikoloni ya kutojiua. Mwandishi anatumia istari ya kisonono kuelezea hali hii.

Tatu, kwa sababu ya unafiki, kiasi kuwa, mtu timamu anaonekana wazimu, mdhalimu kuwa mtetea haki na mwongo kuwa msema ukweli. Kisha, ni kwa sababu ya ujinga uliokita mizizi miongoni mwa wanajamii kiasi cha kuelewa kuwa kunyanyaswa na kuwa maskini ni majaliwa.

Umilikaji wa vyombo vya utawala na tabaka tawala, unapelekea Dzombo kunyimwa haki ya kusikizwa kwa kesi yake na hivyo kuhukumiwa kifo, ambacho kwa ujasiri mkubwa anakiwepa na kujipata katika nchi ya Walenisi alipopata fursa ya kujiendeleza kibinadamu.

Dzombo anafikia kilele cha kujiendeleza kwake anapopata fursa ya kufanya utafiti katika maktaba kuu ya kitaifa katika Walenisi na kisha kuelewa chanzo cha tofauti katika jamii kwa misingi ya kisiasa, kiuchumi, kiitikadi na kijamii, jambo ambalo linamfanya kuazimia kunudi kwao Duniani ili kuwazindua aliowaacha nyuma.

Kwa hivyo matukio haya yote ambayo yanamzunguka Dzombo yanapotiwa na sauti ya nafsi ya tatu ya msimulizi aliye nje ya hadithi na mwenye uwezo wa kujua kila kitu hata ndoto za wahusika.

Hatimaye kuna usimulizi horomo wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi hutoa habari tu na kuwaacha wahusika wenyewe wazungumze bila yeye kuwaingilia na kutoa maelezo au hukumu yake.

Usimulizi wa aina hii tunakumbana nao kwa mara ya kwanza katika sura ya kwanza ukurasa wa sita, baada ya Dzombo kuhukumiwa kifo kwa sayan na sayan kufyatuliwa kwa kutumia nishati ya kinyukilia. Katika ukurasa huu, sauti ya usimulizi inasema:

*“Pia kulikuwa na wale waliofirahishwa na kitendo hicho.
Hawa walisikika wakisema.....”*

Mazungumzo yaliyofuata ni ya wahusika fulani waliomwona Dzombo kama mkosa bahati ambayo wao walikuwa nayo, na pia kama mtu aliye na maneno mengi ambayo kwayo alijichongea kwa kupinga utawala. Hali hii inaonyesha kiwango fulani cha ubinafsi na jinsi jamii ya Dzombo ilivyogawanyika na wanajamii kukolezwa kasumba za kikoloni za mtu kujiamini na kujifikiria kibinafsi.

Aina hii ya usimulizi pia inajitokeza, mwandishi alipotumia mbinu rejeshi na kumrudisha Dzombo hadi mahali alipokuwa akifanya kazi kabla ya kuhukumiwa kifo ambapo alitwa na mwajiri wake kwa kumwambia ndugu yake (Dzombo) kuwa hali yao duni inatokana na kunyonywa na mwajiri wao. Nduguye anaelewa mambo haya kijuu na kumwendea

mwajiri wao na kutaka kumnyonya, katika uk 14 tunasoma:

*"Kwa kuwa ndugu huyu hakuwa anaelewa maana
ya kunyanyaswa, basi yeye keshoye,
alimwendea tajiri wao na kumwambia,
'hebu nami nikunyonye"*

Baada ya hapo, tunaona ni vipi msimulizi anatoa maelezo fulani na kisha kuwaacha wahusika kuzungumza bila kuwaingilia, hali ambayo inapelekea matumizi ya misimbo ya daigesia na homodaigesia kutumika katika usimulizi. Jambo hili huwapa wahusika tofauti fursa ya kutoa maoni yao kuhusu tukio au matukio mbalimbali katika hadithi.

Baadaye Dzombo anaitwa na mwajiri wao, na kuulizwa mambo hayo, alipojaribu kuyakana, ndugu yake akaitwa kuthibitisha kuwa aliambiwa na Dzombo amnyonye mwajiri wao kitu ambacho kilisababisha kufutwa kwake.

Kadhalika hali hii ya usimulizi inajitokeza, baada ya Dzombo kufutwa kazi na kuazimia kuwa mkulima na baadaye mahindi yake kufyekwa kwa madai kuwa aliyapanda bila ushauri wa kitaalamu. Katika ukurasa wa 16, tunaambiwa kuwa, Dzombo aliraukia ofisi ya kilimo ambako tunaona akidaiwa kwa madai kuwa bei ilishuka ghafla na kuwa alikuwa amechukua mbolea

Mwandishi, kwa kutumia usimulizi horomo wa nafsi ya tatu, anawaacha Dzombo na karani anyehusika na kuwalipa wakulima wakizungumza na hivyo kuwapa hadhira fursa ya kujionea ni vipi mafalahi wanavyonyonywa na senkali ambayo kwa hakika inapaswa kuwalinda.

Katika ukurasa 30, Dzombo akiwa anang'angana kukirubani chombo cha kifo (sayari) aligutushwa na sauti fulani humo sayarini, ambazo mwandishi anaziachilia kujibizana bila kuingilia kati. Baada ya majibizano haya, ndipo Dzombo akaambiwa na mtambo-mtu kuwa hilo ni jabali la udhalimu. Sauti hizi zinatufafanulia udhalimu na ubaguzi ambao umekolea ulimwenguni.

Kadhalika usimulizi horomo unatumika Dzombo alipotua Walenisi na kulakiwa na jamaa ya Mzee Mtu-mwenzio na Mama Mtu-maanani na wanao waliomkaribisha kwa vyakula na vinywaji. Kinachofuata ni mazungumzo baina ya Dzombo na wenyeji wake ambapo tunamwona Dzombo akistaajabia mahali hapo na kupachukulia kuwa mbinguni ambapo Mtu-mwenzio ni Mungu, mama Mtu-maanani ni bikira Mariamu, wanao ni manabii na mitume na watoto ni malaika.

Mazungumzo hayo (uk 38-41) yanatuonyesha ulimwengu tofauti na ulio kinyume na ulimwengu anaoufahamu Dzombo kwa kuwaachilia wahusika (Dzombo na wenyeji wake) kuzungumza Mkangi anatutolea picha ya kuaminika kati ya Duniani anakotoka Dzombo na Walenisi, ambapo Walenisi imepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo. Vile vile usimulizi huu (horomo), unafumbata mbinu ya ulinganuzi kwa njia ya kuaminika na kuibua hisi, wahusika wenyewe wanapozungumza na kuonyesha tofauti katika na baina ya nchi hizi mbili.

Mazungumzo mengine ni pale Dzombo aongea na wenyeji kuhusu maandalizi ya safari ya utu. Safari hii ni muhimu kwa jinsi inapaswa kumpitisha Dzombo katika hatua muhimu za kubadilisha utu wake ili awe na hisi na fikira sawa na wawalenisi. Wakiwa safarini inabainika kuwa Dzombo hajafikia ngazi ya wenzake kwa jinsi anavyodhihinisha msimamo wa kikwao (Duniani) kuwa hali ikiwa nzuri ni kwamba ana bahati. Haya yanadhihinka wanapokumbana na hali tofautitofauti wakiwa safarini ambapo wenzao wanampa upendeleo wa kwanza na hivyo anachukulia kuwa ana bahati kushinda wao.

Katika ukurasa 60, wanapokamilisha safari Dzombo anashangaa ni kwa nini wenzake wamedhoofika, na hivyo kufikiria kuwa ni yeye aliwapelekea kudhoofika kwa kujitolea kumpeleka safarini ambapo walikosa bahati. Kushangaa huku ni hatua mojawapo katika ubadilikaji wa Dzombo kuwa binadamu mwenye huruma na mapenzi ambayo yanajitokeza katika uhusiano kati yake na mtu Binti-Fikimi.

Mwandishi anatumia usimulizi maizi kumwingia Dzombo akilini na kutuonyesha anayoyawazia na hapo hapo kubadili hadi usimulizi horomo na kuwaachilia wahusika katika fikira na ndoto za Dzombo kuzungumza. Kwa mfano katika sura ya nne, Dzombo anarudisha fikira zake hadi Duniani na kukumbuka mazungumzo yake na maskini Jeuni kuhusu mafuta ya taa. Katika kisa hiki Dzombo anakumbuka vile walikutana na rafiki yake (maskini Jeuni) baada ya kukosa mafuta aliyemshauni waende 'wakaiwashe taa'. Dzombo alidhani kuwa aliyokuwa nayo ni mafuta ya taa, lakini baada ya kutiwa kwenye kibatan yanalipuka ndipo Dzombo akagundua kuwa hayakuwa mafuta bali ni chang'aa.

Tukio au kisa hiki kinatuonyesha jinsi mfumo wa kikatili unavyoweza kuididimiza jamii hadi kwenye giza la kujisahaulisha uhalisi wenyewe katika maisha. Maskini Jeuni anamkumbusha Dzombo ya kwamba " *taa kwa watu duni kama sisi ni ulevi!*" (uk 74). Mawazo kama haya ni kielelezo cha mawazo ya kujipumbaza ili kukimbia uhalisi wa maisha yalivyo badala ya kujikakamua kugeuza hali hiyo. Mfano huu unamwezesha mwandishi kufumbata ile mbinu ya uandishi inayojulikana kama kisengerenyuma, kwa sababu, tukio hilo liliwahi kufanyika kabla ya Dzombo kuhukumiwa kifo, hatua ambayo ilimpelekea yeye kufika Walenisi ambapo anawazia hayo.

Kadhalika fikira za Dzombo zinaonyeshwa anapofikira kisa alichokishuhudia akiwa kwa mzee Matigasi. Katika kisa hiki wanaume na wanawake wamesawiriwa akilini mwake wakizungumza. Kama tulivyotaja awali, hali hii inawezekana pindi mwandishi anapotumia usimulizi maizi wa nafsi ya tatu kutuonyesha yanayompitikia mhusika katika akili. Katika hali hii tunaonyeshwa majibizano ya wanawake na wanaume katika kundi moja la walevi. Kisa hiki kinafafanua kina cha uozo katika jamii watu wazima wanapotupiana matusi hadharani pamoja na uzembe ulioko watu wanapotumia muda wao mwingi wakinywa pombe. Vile vile tunaelewa ni vipi jamii atokako Dzombo inavyomchukulia mwanamke.

Mfano mwingine unaoonyesha hali hii ya kutumia usimulizi wa aina mbili kwa pamoja ni katika sura ya tano (uk 134 – 5), ndotoni Dzombo anazungumza na mtu Binti – Fikirini kwa urefu kuhusu mapenzi yao. Mifano hii ni ya kipekee kwa jinsi ambavyo inafumbata

usimulizi wa aina mbili kwa pamoja. Hii ni kwa sababu usimulizi maizi unaonyesha ndoto za wahusika, lakini vile vile katika ndoto hiyo, kuna usimulizi horomo tunapowaona wahusika waliosawiriwa ndotoni wakizungumza moja kwa moja hivi kwamba, ungekuwepo ungewaona na kuwasikia

Aidha usimulizi horomo umetumika katika sura ya tisa ambapo Dzombo anapongezwa na Mtu-mwenzio kwa utafiti alioufanya. Katika mazungumzo baina ya Dzombo na wenyeji, tunapata kufahamu kuwa kuna bado hatua moja muhimu na ya mwisho ya kumwelimisha Dzombo ili awe kiumbe razini, na hatua hiyo ni safani ya mapenzoni ambalo ni baraza kuu la ushauri nchini walenisi. Baraza hili limeundwa na wanawake watano, wanaume watano na wawakilishi wa makundi mengine katika jamii. Hii inamaanisha kuwa kuna uwakilishi sawa na demokrasia katika baraza (mapenzoni) la ushauri katika Walenisi kinyume ilivyo katika Fyandusi ya nchi (Duniani) atokako Dzombo

Mazungumzo haya, yanatutolea picha mwafaka ya maisha katika Walenisi ambayo yalitokana na mapinduzi ya Wachuna. Mwandishi analinganisha na kulinganua jamii ya Walenisi na ile ya Dzombo, ambapo anaonyesha kuwa katika jamii ya Walenisi kuna usawa, mapenzi, uhuru wa kusoma na kueneza mawazo mbalimbali, ushirikiano, heshima na mchango mkubwa wa wanawake katika ujenzi wa jamii mpya

Aina nyingine ya usimulizi ni usimulizi tinde wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi anaelezea hisi, mawazo na mambo yanayojulikana na mhusika mmoja au wachache tu mwa waliomo katika ulimwengu wa hadithi. Mwandishi (Mkangi) anapotumia aina hii ya usimulizi, anafaulu kutuonyesha kinaya kinachozunguka matukio fulani katika maisha kwa jinsi ambavyo hadhira inaelekea kuifahamu maana au kidokezi cha hali fulani inayotokea ilhali mhusika mmoja au baadhi ya wahusika hawaelekei kuifahamu hali hiyo. Kwa mfano ndugu yake Dzombo anasawiriwa akiwa haelewi maana ya kunyonya, lakini kwa upande mwingine, Dzombo kama mwana harakati - anaelewa na pia tabaka tawala linaelewa kwa vile ndilo linalonyonya wengine.

Dzombo anapotua walenisi, tunaona kuwa hapa elewi mahala hapo, na badala yake

anapachukulia kama ahera, lakini wenyeji wake wanaelewa ndiyo sababu wanampeleka kwa safari ya utu. Ajabu ni kwamba hata haelewi ni kwa nini anapewa upendeleo wa kwanza wakiwa safanni, jambo ambalo wenyeji wake wanalielewa vizuri. Akiwa waleni, Dzombo anashangaa na kukosa kuelewa ni kwa vipi waleni ilikuwa imepiga hatua kimaendeleo hadi alipopewa fursa ya kutafiti hali hiyo.

Katika visa vya moto, uchawi na mabavu, watu ambao ni wahusika wa kutajwa (hawashiriki hadithini) hawaelewi maana ya visa hivi, lakini mabavu, mchawi na msasi wanaelewa maana ya visa hivi.

Kwa kuhitimisha, tunaweza kusema kuwa sura hii inajadili swala la mtazamo na wasimulizi katika riwaya ya waleni. Kutambua wasimulizi pia hujumlisha ufasiri wa hali na mitazamo yao. Katika riwaya hii Mkangi, anabadili mitazamo ya usimulizi. Ni muhimu kutambua kubadili huku kama wanavyosema Scholes na Kellog kuwa msimulizi na hadithi huenda pamoja katika uwasilishi na ukuzaji wa simulizi. Kulingana nao

*"Sanaa ya simulizi huhitaji hadithi na msimulizi
Katika uhusiano kati ya msimulizi na hadithi, na
ule uhusiano mwingine kati ya msimulizi na hadithi,
ndiko kuna kiini cha sanaa ya simulizi." (240)*

Hivyo basi, kama tulivyodokeza hapo awali, mwandishi anabadili mitazamo na kutumia sauti mbalimbali za usimulizi. Kwa mfano tumeona jinsi usimulizi na msimulizi wa nafsi ya kwanza anavyosimulia matukio mbalimbali hasa kuhusu nchi ya Waleni. Haya ni katika utafiti wa Dzombo alioufanya nchini Waleni. Hata hivyo hadithi inavyosonga, usimulizi huu unabadilika na kuwa wa nafasi ya tatu ambao unampa mwandishi uwezo wa kuelezea mambo ambayo msimulizi wa nafsi ya kwanza hawezi.

Kwa ujumla usimulizi na wasimulizi wa nafsi ya tatu katika hali na aina zao mbalimbali ndio wametawala katika hadithi ya Waleni, ambapo sauti mbalimbali za usimulizi zinashindana kila moja ilitaka kusikika. Kwa kufanya hivi, mwandishi anajadili maudhui

tofautitofauti katika nwaya hii nakutoa maelezo mbalimbali kuhusu matukio mbalimbali kwa mitazamo tofautitofauti.

Tunaweza kusema kuwa sura hii inajibu swali la ni nani anasimulia hadithi. Sababu yake ni kwamba, mtazamo wa hadithi unakwenda sambamba na msimulizi, ingawa tunajua kuwa sauti fulani ya usimulizi inaweza kusimulia matukio fulani kwa mtazamo wa mwingine, kama tunavyoona katika sentensi ya kwanza na kwingine kwingi katika nwaya hii.

Vile vile kwa kushughulikia mtazamo kama kipengee cha usimulizi tumeona kwamba kipengee cha maudhui pia kinaathirwa na mitazamo mingi ambayo inazua miktadha tofauti na maana mbalimbali.

Kadhalika tumeona kuwa hali halisi na ya kisaikolojia ya wasimulizi na matukio katika nchi bunilizi za Walenisi na duniani (atokako Dzombo) huathiri ufahamu wao kwa matukio hayo. Kwa mfano, matatizo ya kisiasa, haki na ukweli yanaeleweka kwa njia mbalimbali kutegemea tabaka la kijamii analojitambua nalo msimulizi. Hivyo hivyo ufahamu wa maswala ya kijinsia unategemea anakotoka msimulizi. Sababu ni kuwa nchi za Walenisi na Duniani zimesawirwa kiulinganuzi.

SURA YA TATU

UNENAJI NA FIKIRA

Katika nwaya, wahasika aghalabu huzungumza na wanapofanya hivyo, huwa wamejitoma katika usemi halisi kwa kutumia viwakilishi nafsi ya kwanza. Hali ikiwa hivyo mtazamo wa hadithi utakuwa wa ndani kama tulivyoona katika sura ya pili.

Kadhalika, mwanariwaya anaweza kuwasilisha unenaji katika usemi wa taarifa anapotumia viwakilishi vya nafsi ya tatu. Usemi wa taarifa unakwendana na usimulizi wa nafsi ya tatu unaoangaza hadithi kwa mtazamo wa nje ambapo kuna wakala aliye nje ya hadithi akisimulia matukio ya hadithi kulingana na alivyoyaona.

Mwandishi wa nwaya aghlabu hutumia mikabala yote miwili ya usemi halisi na usemi wa taarifa kwa kubadili kutoka mmoja hadi mwingine. Kadhalika mikabala hii inapotumika, inazua mikabala mingine zaidi kama tutakavyoona baadaye.

Tofauti kati ya usemi halisi na usemi wa taarifa pamoja na kubadili kutoka hali moja hadi nyingine na ni vipi usemi halisi unavyotofautiana, na kufanana na mazungumzo ya kila siku pamoja na ufasiri wa mabadiliko hayo na msomaji ndicho kiini cha sura hii.

Kimsingi, tofauti kati ya usemi halisi na usemi wa taarifa ni kuwa, tunapotumia usemi halisi kunpoti kilichosemwa na mwingine, huwa tunanukuu maneno yale moja kwa moja, ilhali katika usemi wa taarifa huwa tunasema kilichosemwa na mtu mwingine kwa kutumia maneno yetu wenyewe

Uhusiano uliopo baina ya aina hizi za unenaji unajitokeza vizuri tunapogeza usemi halisi hadi usemi wa taarifa. Kwa mfano baada ya Dzombo kuhukumwa kifo, kuna mazungumzo baina ya watu fulani kuhusu yaliyomsibu Dzombo ambapo tunasoma:

(a) *Hawa walisikika wakisema, "hii ndiyo dawa ya maneno mengi." (06).*

Senstensi hii ikigeuzwa hadi usemi wa taanfa, itakuwa.

(b) *Hao Walisikika wakisema kuwa hiyo ndiyo dawa ya maneno mengi.*

Katika sentensi hizo hapo juu yaani 'a' na 'b' mabadiliko yafuatayo yametokea:

Kwanza kabisa, alama za mtajo zinazoonyesha kwamba kuna unukuzi na pia zinazoonyesha kuwa nukuu hategemezwi kisarufi kwa kitenzi arifu, 'sema' zimeondolewa na hivyo kufanya usemi wa taanfa kutegemea kitenzi arifu.

Pili, utegemezi umetangulizwa na kuonyeshwa kwa kutumia kiunganishi kitegemezi 'kuwa' na mwisho ni kuwa, kivumishi kionyeshi 'hawa' kinabadilika na kuwa 'hao' kuonyesha uhusiano wa kimasafa baina ya mnenaji na wanaotajwa. Hatimaye kionyeshi 'hii' kinabadilika na kuwa 'hiyo' kwa sababu za kimasafa.

Athan ya mabadiliko haya kulingana na Leech na Short ni kutoa sifa zote zinazohusiana na usemi wa taanfa egemezi pekee na kutegemeza usemi wa taanfa kwa kitenzi arifu 'sema' kilichoko katika usemi halisi (1981:319).

Katika mfano uliopo hapo juu, wakati na mahali ambapo matukio katika usemi halisi na usemi wa taanfa yanatokea ni tofauti lakini elementi nyingine muhimu hazijabadilika. Kwa mfano:

"Hii ndiyo dawa ya maneno mengi."

ni maneno katika usemi halisi yaliyotamkwa mahali sayan ilikofyatuliwa na aliyetamka alifanya hivyo wakati huo na mahali hapo Tukumbuke kuwa neno 'hii' halawezi

kutumika katika usemi wa taarifa kwa jinsi ambavyo linaonyesha uhusiano wa karibu kimasafa na mnenaji na hivyo inafaa litumike katika usemi halisi kama ambavyo limetumika. Kwa hivyo inahalisi kusema kuwa mfumo wa uwasilishaji wa unenaji unaafikiwa sio tu kwa kuwepo kwa sifa rasmi za kiisimu.

"bali pia kwa uelewa wetu wa matumizi ya miktadha mingine isiyo ya kiisimu " (Leech na Short: 320)

Athari inayotokea usemi wa taarifa unapotumika kuwasilisha unenaji ni kuwa anayeripoti anaingilia kati ya dayolojia au malumbano kama mfasiri kati ya anayezungumza anayezungumziwa. Kadhalika badala ya kunukuu moja kwa moja vile unenaji ulivyotokea, kilichotokea kinaripotiwa kwa maneno ya anayenpoti na hivyo kinachonpotiwa kuingizwa katika simulizi.

Tofauti hii inaweza kujitokeza vizuri kwa kile anayeripoti anataka kuonyesha. Kwa mfano akiripoti katika usemi halisi, huwa anadai kuwa anaripoti kwa uaminifu, kilichosemwa na pia maumbo ya maneno jinsi yalivyotumiwa kutoa kauli ile. Mkangi amewasilisha unenaji wa aina hii anapomsawiri Dzombo akizungumza na karani wa idara ya kilimo, na anapozungumza mambo mbalimbali na wenyeji wake akiwa nchini Walenisi.

Kwa upande mwingine, usemi wa taarifa unapotumika, mwandishi huwa anataka kuonyesha kilichosemwa, na matokeo ni kuwa, baadhi ya maneno ya usemi wa taarifa yanaweza kubadilika bila kubadilisha maana ya kauli hata kidogo. Kwa mfano njeo ya kitenzi, vionyeshi na hata vielezi vya mahali vinanaweza kubadilika lakini maana ya kauli ibakie ile ile kama tulivyoona hapo awali.

Mfano ambao tumeujadili hapo juu, unahusisha mabadiliko ya kisintaksia na kileksika pekee ambapo katika usemi halisi anayenpoti hudai kuwa anaripoti kwa uaminifu muundo wa kisintaksia na kileksika wa mnenaji halisi. Pia muundo wa kuaminika hata

zaidi unaweza kutolewa kwa kuwakilisha iwezekanovyo matamshi ya kauli au sentensi awali kama Leech na Short kuwa (1981:321) wanavyosema:

*“katika unenaji ubora wa sauti unaweza kuigwa
ili kuonyesha hisia za mnenaji kama vile kiburi ili
kusisitiza thamani ya kuwasiliana”*

Kwa mfano Dzombo anapohukumiwa kifo, tunamwona mnyongaji ‘halali’ akimwambia, *“Dzombo, kifo ni kifo na hakuna kurudi nyuma tena.”* (05).

Kauli hii inaweza kusemwa kwa njia mbili tofauti ili kuonyesha kuwa ni kauli tu au kuonyesha kuwa ni shuruti au anamlazimisha angie sayanni.

Kadhalika, lafudhi ya tabaka au eneo fulani inaweza kuigwa, lakini waandishi wengi wa nwaya hutumia othografia iliyokubalika kudokeza mawasiliano. Hali hii inajitokeza Dzombo akiwa Walenisi akizungumza na wenyeji wake.

*“Aaa, samahani sana. Yes maana yake ni
kusema ‘ndio’. Pia huenda ikatumika kumaanisha
mmmh ... mmmh ... aha ... aha na kadhalika”
“Na hii ‘aiamusoli” Mtu – Binti I’ikirini akamkumbusha”. (87).*

Mfano mwingine ni katika ukurasa wa 185 mwandishi anaposawin kisa cha Medza na mwanawe jinsi alivyokosa huduma ya matibabu daktari anapomwambia *“Jaribu tena kesho mama”* matamshi ya daktari yanaweza kuchukuliwa kama kauli tu au kutojali maisha ya akina yahe kama ilivyokuwa kawaida Duniani alikotoka Dzombo

Mifano ya kuonyesha hali hii ni mingi katika hadithi na haiwezekani tuitoe yote kwa sababu athari, sababu na maana ya kutumiwa na mwandishi ni sawa. Ni muhimu

kudokeza kwamba waandishi wa riwaya wanapowasilisha unenaji kwa njia yoyote ile, huwa wanafanya hivyo ili kuradidi maudhui katika hadithi.

Kwa mfano maudhui ya ukombozi na uanaharakati yameradidiwa na mwandishi anapomsawiri Dzombo katika mazungumzo (usemi halisi) na mwajiri wake na baadaye na karani katika ofisi ya kilimo.

Vivyo hivyo maudhui ya ubinafsi yameradidiwa Dzombo anaposawirwa katika mazungumzo na baadhi ya wenyeji wake wakiwa safarini kupima utu wake.

Usemi halisi unapotumika maneno kama yalivyotamkwa hufungiwa katika alama za mtajo kisha kufuatwa na ushawishi (tagging) kuonyehsa ni nani alisema maneno yale na vile vile kuonyesha kuwepo kwa msimulizi. Chembilecho Barry (1993:238):

*“matumizi ya usemi halisi ni ushahidi tosha wa
kuwepo kwa msimulizi karibu na wahusika
wanaozungumza.”*

Hali ni kinyume mwandishi anawaposilisha unenaji katika usemi wa taarifa ambapo maneno hayatolewi moja kwa moja kama yalivyosemwa, badala yake yanapotiwa na msimulizi wa nafsi ya tatu kama tulivyosema awali. Katika hali hii msomaji huyaona matukio yanayosimuliwa kwa mbali. Sababu yake ni kwamba kama wanavyosema Leech na Short (1981:321):

*“mahali na wakati wa matukio katika usemi wa taarifa
ni tofauti na ilivyo katika usemi halisi kwa
jinsi ambavyo vionyeshi na deiksisi mahali hubadilika”*

Mbali na usemi halisi na usemi wa taarifa, mwanariwaya huwa na mifumo mingine ya unenaji. Nayo ni pamoja na, mfumo ulio wazi au huru zaidi kushinda usemi halisi,

mfumo fiche au funge zaidi kuliko usemi wa taarifa na mfumo ulio mchanganyo kati ya usemi halisi na usemi wa taarifa.

Usemi halisi una sifa mbili kuu zinazoonyesha kuwepo kimwili kwa msimulizi, yaani alama za mtajo na kishazi tangulizi kinachoanfu. Ikiwa zote au moja ya sifa hizi imeondolewa matokeo ni mfumo ulio huru unaojulikana kama usemi halisi huru, ambapo wahusika wanaongea na hadhira moja kwa moja bila msimulizi kuingilia kati.

Hali hii inajitokeza Dzombo akiwa sayanni kuelekea anga za mbali kunapotokea sauti alipokumbana na jabali la udhalimu. Sauti hizi zinapotishana, Mkangi anatumia usemi halisi huru kwa vile sifa moja kuu ya usemi halisi imeondolewa yaani kishazi tangulizi kinachoanfu hakipo (30 – 31). Mfano mwingine ni katika ukurasa wa 37, Dzombo anapotua nchini Walenisi na kukaribishwa na wenyeji wake. Katika ukurasa huu, tunasoma,

"Karibu mtu-Dzombo"

"asanteni sana"

"Je, safari ilikuwaje?"

"Ngumu"

"Na huko utokako?"

"moto...."

Katika mfano huu, kishazi tangulizi kimeondolewa lakini alama za mtajo zimebaki na hivyo kuunda usemi halisi huru. Kishazi kitangulizi kinapoondolewa, athari yake ni kuharakisha dayolojia kati ya wahusika. Athari nyingie ni kuwa msomaji anaweza kutoa hukumu isiyosahihi kuhusu wahusika. Hata hivyo ni kweli anaposema Barry (1993:237):

*"muundo huu unaweza kuzua utata kuelewa ni nani
amesema nini kati ya wahusika ikiwa kishazi
tangulizi hakipo"*

Uwezekano wa muundo ulio wa moja kwa moja zaidi hutokea katika sentensi ambazo huonyesha kuwa kitendo au vitendo vya unenaji vimefanyika lakini msimulizi hajishughulishi na kutoa maana ya kilichosemwa au hata kuonyesha mpangilio wa maneno ya kilichosemwa. Kwa mfano Mtu – Binti Fikiri anapozungumza na Dzombo anasema,

"Waumwa?" Sauti yake ilikuwa imejaa huruma. (64).

Kauli hii inaweza kusemwa kwa njia nyingine tofauti kama ifuatavyo,

Alimwuliza swali au

alimwonea huruma – ili kutoa maelezo mafupi ya kauli ya awali. Hali kama hii ya unenaji inajulikana kama ripoti simulizi ya vitendo vya unenaji.

Aina hii ya unenaji ni muhimu kwa kutoa muhtasari wa mazungumzo marefu yasiyo muhimu. Mwanariwaya anaporipoti kutokea kwa tukio fulani huwa anatumia kuona tukio hilo katika mtazamo wake. Hivi ndivyo matukio mengi katika *Walenisi* yameripotiwa mwandishi anapotumia wakala aliye nje ya hadithi kusimulia matukio hadithini.

Hata hivyo, unenaji unabadilika kutoka usemi halisi fonge wakati kuna kuingilia kati kwa mwandishi katika mazungumzo kunapozidi kupungua na kisha kuwa na muundo huru wa usemi halisi anapoacha wahusika kuzungumza bila kuwaingilia kama tulivyosema na kutoa mifano hapo awali.

Aina nyingine ya unenaji ni usemi wa taarifa huru ambao aghalabu huchukuliwa kama mfumo dhahiri wa usemi wa taarifa. Sifa yake ya kimsingi kinyume na usemi wa taarifa ni kuwa kishazi anfu huwa kimeondolewa, lakini njeo na viwakilishi ni vile vinavyohusishwa na usemi wa taarifa, kwa mfano sentensi;

"Jaribu tena kesho mama" Daktari akanwambia. (185) inaweza kuchukua mifumo ifuatayo ya usemi wa taarifa huru:

- a) angerudi hapo tena siku itakayofuata
- b) Atarudi hapo kujaribu tena.
- c) Atakuja hapo kujaribu tena

Sentensi (a) hapo juu ni mfumo wa taarifa ulio huru kwa sababu kishazi anfu kimeondolewa na hivyo kuruhusu kishazi arifiwa ambacho hutegemezwa kwa muundo taarifa kuchukua baadhi ya sifa zinazohusishwa na usemi halisi.

Usemi wa taarifa ulio huru hutokea katika muktadha wa sentensi za ripoti simulizi ambapo msimulizi wa nafsi ya tatu anazidi kusimulia akitumia wakati uliopita hali ambayo Mkangi ametumia kila anapowasilisha hadithi yake katika usimulizi wa nafsi ya tatu. Leech na Short (1981:325) wanasema:

"sifa za kuwepo kwa usemi huu katika riwaya ni kuwepo kwa viwakilishi vya nafsi ya tatu na njeo ya wakati uliopita inayoingiliana na umbo la ripoti simulizi ya kuonyesha utaarifa pamoja na sifa kadha ya kinishi na kanushi kuonyesha kuwa ni huru."

Kwa hivyo kama tulivyosema ni umbo huru la kuripoti katika usemi wa taarifa.

Aina hii ya unenaji imetawala katika hadithi ya *Walenisi* msimulizi anavyotupitisha katika mahali mbalimbali akisimulia yaliyomsibu Dzombo tangu kuhukumwa kifo kwa sayari, jinsi alivyokirubani chombo (sayari) cha kifo hadi alipotua Walenisi. Kadhalika Dzombo akiwa Walenisi, msimulizi anamfuatilia kwa karibu na kusimulia jinsi alivyostaajabia nchi hiyo, alivyokaribishwa na kutembezwa katika maeneo yote ya Walenisi na baadaye kumwoa Mtu-Binti Fikinni na kurudi naye duniani. Mkangi anafanya hivi kwa kutumia msimulizi maizi wa nafsi ya tatu anayetumia viwakilishi vya nafsi ya tatu na njeo ya wakati uliopita

Usemi wa taarifa ulio huru, humpa mwandishi uwezo wa kuongeza radha kwa maneno ya wahusika, na pia kuweka usimulizi katika hali ya mwinigiliano kati ya wahusika na mwandishi na hivyo kuonyesha kinaya cha kile kinachozungumziwa na wahusika.

Kwa hivyo usemi huu wa taarifa unatumia njeo ya wakati uliopita na viwakilishi vya nafsi ya tatu kama ambavyo tumekwishataja. Ni muhimu kudokeza kuwa uteuzi wa viwakilishi na njeo lazima uwiane na muundo wa usimulizi kunapotokea umbo la usemi wa taarifa huru.

Inaeleweka kwamba wakati uliopo unaamriwa na mtindo wa usimulizi. Kwa hivyo kinachoonyesha kuwa taarifa fulani iko katika usemi wa taarifa ulio huru ni viwakilishi vya nafsi ya tatu na matumizi mwafaka ya alama za mtajo kwa vitenzi.

Athan mojawapo ya matumizi ya usemi wa taarifa huru ni kuwa huleta kinaya. Kulingana na Lecch na Short (1981:334):

"Kinaya hutokea kwa sababu usemi wa taarifa huru huwa unkuangaliwa kama usemi ambao sauti ya mwandishi inaingika kati ya msomaji na kile wahusika wanazungumza, hivyo kurefusha masafa kati ya msomaji na mazungumzo ya wahusika."

Hali hii inabainika zaidi tukichukulia kuwa usemi halisi ndio msingi wa unenaji. Kwa mfano katika sura ya tatu Dzombo anakaribishwa Walenisi na mvulana mmoja akamwuliza kama angekunywa chai ya aina gani, na yafuatayo ni mazungumzo yao:

"Ya mkoko?"

"Maziwa."

"Ya moto ama ya baridi?"

"Ya moto."

"Na sukari je?"

"vijiko viwili!! Akapewa kikombe chake na mmoja"

*wa wale wasichana akamsongezea
kisini cha maandazi (44).*

Tunapoiangalia dayolojia iliyopo hapo juu, tunaona kuwa imewasilishwa katika semi wa taarifa huru ambapo wahusika wanazungumza moja kwa moja bila matumizi ya kitenzi anifu. Lakini Dzombo anapojibu swali la mwisho kuwa angetaka vijiko viwili vya sukari, sauti ya mwandishi (msimulizi) inaingilia kati ya msomaji na wahusika na kurefusha masafa kati yao na hivyo kuonyesha kinaya kuwa sio wahusika wanaozungumza kihakika bali msimulizi aliwaiga tu na ndio sababu anasema, "akapewa kikombe chake na mmoja wa wale wasichana akamsongezea kisini cha maandazi."

Kadhalika kwa kutofautisha mbinu za unenaji katika uwasilishi wa unenaji, mwandishi anafaulu kumtia mhusika mmoja katika hali ya mhusika mwingine na kumpelekea msomaji kuelewa fikira za wahusika tofauti kuhusiana na ujumbe fulani.

Hali hii tunaona katika sehemu mbalimbali za riwaya kwa mfano katika sura ya nane Dzombo akiwa katika safari ya mapenzoni, mwandishi anasema,

*"akiyatembeza macho yake tena kwa kila mjumbe kwa
uhakikisho, Dzombo mara akamwona yule mama
akipumua kama mtu ambaye amesamehewa kunyongwa.
Baada ya wenzake kumwambia hakukuwa hata na
mtu mmoja wa kiwalenisi ambaye hakuwa akienda
mapakuuji kwa sababu yoyote ile ya kijamii." (211).*

Katika mfano huu, jibu limetengwa kimasafa kwa kuwasilishwa katika usemi wa taarifa huru, na hisia kiimbo kuisisitizwa kwa kuingizwa kwa mama na mtu. Katika muktadha huu athari yake si ya kinaya, lakini ni kumtia mhusika mmoja katika hali ya mwingine kama tulivyotaja hapo awali.

Mifano zaidi ya hali hii ni pamoja na ule wa Dzombo kuhukumiwa kifo na watu mbalimbali kuwa na maoni tofauti tofauti kuhusu hukumu hiyo na hali yake Dzombo akiwa sayarini.

Kadhalika Dzombo baada ya kumwoa Mtu – Binti Fikirini tunaona jinsi anavyohuzunika akiwakumbuka watu wa duniani alikotoka. Katika ukurasa 216, tunasoma:

*“Vile wateswavyo, wanyanyaswavyo, waumizwavyo,
wapumbazwavyo, na kwa jumla kuishi katika hali
ya uzima mauti ukweli – uongo wanaopewa na
Wachuna wa huko.”*

Vilevile mifano hii inaonyesha ni vipi usemi wa taarifa ulio huru unatofautiana na aina nyingine za unenaji ili kumwezesha mwandishi kudhibiti mazungumzo ya wahusika kulingana na jukumu na fikira zao.

Tunaweza kuhitimisha kuhusu unenaji kwa kuwarejelea Leech na Short(1981:326) wanaosema :

*“kabadili mikabala ya unenaji kunaweza
kutumika kumfanya msomaji kumhurumia
mhusika au wahusika fulani kuliko wengine.”*

Katika riwaya hii, tunaposoma tunamhurumia Dzombo na kumchukia mnyongaji. Vivyo hivyo tunaposoma kisa cha mapacha tunamhurumia Medza na kumchukia daktari na kundi lote la Wachuna.

Aidha usemi wa taarifa ulio huru unatumika kufanikisha kinaya, kwa sababu kutokea kwake katika ile sehemu ya taarifa ya usemi halisi huruhusu matumizi ya mitazamo miwili, yaani mtazamo wa m(wa) husika na wa mwandishi. Kadhalika usemi huu unatumika kwa kufasiri mazungumzo na pia kama kipengee cha mtindo.

Mbali na unenaji, mwandishi wa riwaya vilevile huwasilisha fikira za wahusika wake kuhusiana na mambo na matukio mbalimbali katika ulimwengu wa hadithi. Leech an Short (1981:237) wanadai kuwa:

"wandishi wengi bora wa karne za kumi na tisa na ishirini wamejishughulisha kwa kina na usimulizi wa unenaji nafsi. Sababu yenyewe ni kuwa walitaka kuwasilisha ni vipi fikira zinavyompitikia mhusika katika akili na hivyo uwasilishi wa fikira umekuja kuhusishwa na kile kinachojulikana kama mkondo wa uandishi wa ufahamu nafsi."

Ni vigumu kuona kinachompitikia mhusika akilini mwake, lakini kwa matumizi ya mbinu ya uzungumzi nafsia, mwandishi anaweza kubaini vitendo na fikira za mhusika. Hii ni mbinu inayotuangazia mivutano ya kimawazo inavyompitikia mhusika. Aghalabu uzungumzi nafsia hutufichulia fikira na mawazo ya ndani ya mhusika, hofu zake, matarajio yake na huweza kuwa mojawapo ya mbinu zinazotumiwa na mwandishi kumkuza mhusika. Mfano mzuri wa uzungumzi nafsia ni pale Dzombo anapokuwa sayanni (uk. 10).

*"Hivyo vingine vingojee, kwani natazamia kula
mana hivi karibuni " Akajisemea moyoni.*

Mfano mwingine wa uzungumzi nafsia ni pamoja na wakati Dzombo akanabishwa huko Walenisi na wenyeji wake." (uk 38).

*"Huku akiingia, Dzombo alikuwa akiwaza, leo utumwa
wa njaa na kuu naenda kuubwaga milele..."*

Haya ni mawazo yaliyokuwa yakimpitikia Dzombo akilini mwake na mwandishi alifaulu kuyaonyesha kwa msomaji kwa kumsawiri mhusika akiwa anajisemea moyoni, kadhalika hali hii inajitokeza Dzombo anapostaajabia mandhari ya mbinguni (Walenisi) na kusema

“mamangu! Nimepotea njia” akajisemea tu Vile vile katika ukurasa wa 57, Dzombo akifikina juu ya ukanmu wa Mtu-Binti Fikinni akajiambia

“na kumbe hawa wanawake wa huku ni kama wa kwetu – ya kuhakikisha kuwa wanaume wameshiba kwanza kabla ya wao wenyewe! Bahati gani hii Dzombo? Nilikiwa nimeshakufa! Aa, kweli bahati ya mwenzio usulalie nje!”

Kwa kumsawiri Dzombo akiwa katika uzungumzi nafsia, Mkangi anatuwezesha kupata fikira na mawazo ya Dzombo kuhusu wanawake, yaani mtazamo wa kiduniani kwamba wanawake wanawatumikia wanaume. Kwa hivyo Mkangi amemsawiri Dzombo akiwa katika hali ya kujizungumzia katika mahali mbalimbali hadithini.

Mbali na uzungumzi nafsia, waandishi wana mbinu mbalimbali za kuweza kutambua kilicho katika akili ya wahusika. Mbinu hizo ni sawa na zile za uwasilishaji wa unenaji. Nazo ni pamoja na fikira za taarifa zilizo huru, kuripoti anachofikina mhusika na kuonyesha tajriba na ufahamu wa mhusika kuhusu fikira hizo papo kwa papo.

Imekwishatajwa kwamba, njia ambazo mwandishi anaweza kutumia kuwasilisha fikira za wahusika ni sawa na zile za kuwasilisha unenaji, na kama wanavyosema Leech na Short (1981: 237) na Barry (1995: 239) zimebainishwa miongoni mwao kwa njia sawa na mbinu za kuwasilisha unenaji.

Mbinu hizo ni pamoja na kuwasilisha fikira kwa kutumia usemi halisi huru na fikira hizi zinajulikana kama fikira halisi huru. Katika muktadha huu, fikira zinaonyeshwa kwa kutumia usemi halisi ulio huru, lakini kishazi tangulizi na alama za mtajo huwa vimeondolewa. Mwandishi anaweza kutumia mbinu zote ambazo zimewahi kujulikana kuwasilisha fikira au atumie baadhi yazo. Kwa mfano Mkangi hakutumia mbinu hii ya fikira halisi huru.

Kadhalika kuna fikira halisi za moja kwa moja. Hizi ni fikira zinazoonyeshwa kwa kutumia usemi halisi ambapo kuna matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza pamoja na alama za mtajo. Kwa mfano katika sura ya pili, mazungumzo kati ya nduguye Dzombo na mwajiri wake yanadhihirisha fikira halisi za moja kwa moja kwa jinsi ambavyo viwakilishi vya nafsi ya kwanza pamoja na alama za mtajo vimetumika. Katika ukurasa wa 14, tunasoma.

"Eti wasemaji? Tajiri akamwuliza."

"nimeambiwa kwamba nikikukunyonya,

basi nami natakiwa na hali ya kuvutia kama yako."

Akajieleza. "Kwani waniona niko na matiti."

Tajiri akamwuliza kwa hasira

"sijui mimi, Lakini nimeambiwa hivyo tu."

Akajieleza kwa unyenyekevu

Kiambishi 'ni' ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza katika umoja 'mimi' vilevile ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza katika umoja ambavyo vimetumika pamoja na alama za mtajo kuonyesha kuwa fikira za nduguye Dzombo na mwajiri wake ni halisi na za moja kwa moja

Hali hii pia inadhihirika Dzombo anapoitwa na mwajiri kuelezea ni kwa nini anamchochea ndugu yake ambaye kulingana na mwajiri ni mfanyikazi mtuifu.

Mkangi amewasiri Dzombo na mwajiri wake wakitumia viwakilishi nafsi ya kwanza wanapozungumza na hivyo kutuonyesha fikira zao kwa njia halisi na ya moja kwa moja.

Fikira hizi zinaonyesha Dzombo kama mwanaharakati anayeelewa haki zake na vilevile aliyejitolea kuwazindua watu wengine. Mwajiri naye kwa upande mwingine ni katili na mnyonyaji anayeogopa watu waliq'na mawazo ya kiharakati kama Dzombo jambo ambalo lilimfanya amfute kazi.

Kadhalika, kama tulivyoona hapo awali, mazungumzo kati ya Dzombo na karani wa kilimo yanatuonyesha fikira za kiudadisi za Dzombo anapotaka kujua ni nani anayeweka bei ya mazao yao. Vivyo hivyo karani wa kilimo ni kibaraka cha utawala kandamizi unaowanyonya maskini bila huruma.

Fikira hizi vilevile zimetumika Dzombo anapokumbuka kisa cha maskini Jeuri. Mazungumzo kati ya maskini Jeuri na Dzombo ni halisi na ya moja kwa moja ambapo mawazo ya Jeuri ni ya kujipumbaza ili kuukimbia uhalisi wa maisha ulivyo.

Katika kurasa za 30 – 31 kuna sauti zinazosikika zikijibizana sayarini ambazo zinafumbata fikira huru za moja kwa moja jinsi usemi halisi huru ulivyotumika na hivyo kuwasilisha fikira za udhalimu zilizowatawala watu wa Duniani. Tulivyotaja hapo awali ni kuwa, unenaji na fikira ndio msingi wa uradidi wa maudhui. Kwa hivyo sauti hizo ambazo ziko katika usemi halisi, zinaradidi maudhui ya udhalimu uliojengeka katika msingi wa ubaguzi wa aina mbalimbali kama vile wa kijinsia, kidini na wa rangi.

Mbali na fikira halisi za moja kwa moja, Mkangi vilevile aliwasilisha fikira taarifa zilizo huru kwa kutumia usemi wa taarifa ambapo njeo ya kitenzi hubadilika kutoka wakati uliopo hadi wakati uliopita na kiwakilishi cha nafsi ya kwanza kubadilika hadi nafsi ya tatu. Vilevile kishazi anfu huwa kimedondoshwa lakini afama za kuuliza swali hubakia kwa mfano katika ukurasa wa 207, tunasoma:

*“mara Dzombo akaona Buku likifunguliwa na mwili wake
wote akamfa ganzi... kumbe kweli kuna siku ya hukumu?”*

Mwandishi anatupa fikira na taswira ilitiyomjia Dzombo kuwa pale mapenzoni ni mbinguni, na kutumia taswira hii ya mbinguni kuwakumbusha wasomaji kuwa uwezo wa kujenga jamii yenye usawa, uhuru, haki, na ukweli wanao wanajamii. Mifano mingine zaidi ya fikira za aina hii ni katika sura ya nane ambapo tunasoma:

"si kuishi, binadamu – au kumbe chochote kile, sharti ale ashibe?" "Si Kuishi, mtu sharti ajitumikishe kwa juhudi zake kwa kuwa mtu ni kazi?" "nani alitoka tumboni mwa mamake amevaa nguo?" (uk 172).

Hizi ni fikira taanfa zilizo huru, zinazowasilishwa kwa umbo la maswali anayoyauliza Dzombo baada ya kugundua hila na njama za Wachuna za kuwaaminisha maskini kuwa matatizo yao ni majaliwa au ya kijaala

Mkangi vilevile aliwasilisha fikira taanfa katika hadithi yake. Hizi ni fikira zinazoonyeshwa kwa kutumia usemi wa taanfa hasa kwa kutegemeza kishazi huru kwa kishazi tangulizi. Aina hizi za fikira zimetawala hadithi kwa jinsi zinavyokwenda pamoja na usimulizi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi yupo nje ya hadithi.

Dzombo akiwa Walenisi alijawa na hamu ya kutaka kuelewa ni vipi Wachuna walivyoanzisha uchuna na ni vipi waliondoshwa na Walenisi. Badala ya kujibiwa.

Walenisi walimpa fursa ya kutafiti mambo haya katika maktaba ya kitaifa ya Walenisi. Anapotoa matokeo ya utafiti wake, anaanza kwa nafsi ya kwanza lakini baadaye anabadili na kutumia nafsi ya tatu ambayo inamwezesha kuwafuata Wachuna na kuripoti tabia, vitendo na mienendo yao. Hali hii inatokea kwa sababu ya ufinyu wa mtazamo wa ndani, yaani usimulizi wa nafsi ya kwanza

Kupitia Dzombo, Mkangi anafaulu kusawiri na kuwasilisha fikira za Wachuna na anafanya hivyo kwa kutumia usemi wa taanfa ambapo kiwakilishi 'a' cha nafsi ya tatu katika umoja kimetumika. Kadhalika kiwakilisha 'wa' cha nafsi ya tatu katika wingi kimetumika.

Fikira taanfa za Wachuna zinajitokeza Dzombo anaponpoti kuhusu asili ya Wachuna kwa kutumia visa mbalimbali. Visa hivi ni pamoja na kile cha moto, mabavu, mchawi na cha mapacha ambavyo vinafafanua vile Wachuna walivyowalaghai watu na kujitajirisha. Hata hivyo kisa cha mapacha vilevile kinaelezea tofauti na uhasama kati ya ndugu na

ndugu, jambo ambalo lina asili yake katika Uchuna. Kwa mfano katika ukurasa wa 154 tinasoma,

"Siku moja mtu ambaye alijulika kwa jina la moto, alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbiyu."

Katika dondoo hilo hapo juu, Dzombo ananpoti kuhusu Moto ambaye alizua nasaba mojawapo ya Uchuna kwa kutumia kiwakilishi 'a' cha nafsi ya tatu na 'li' ya wakati uliopita katika vitenzi. Hali hii inaonyesha kuwa usemi wa taarifa unatumika na hivyo kupelekea kuwepo kwa fikira taarifa.

Vilevile, ananpoti kuhusu kisa kilichozua Wachuna wa ukoo wa uganga kwa usemi wa taarifa, na kufanya fikira hizo ziwe fikira taarifa kama tulivyotaja hapo awali.

Unenaji na fikira na jinsi ya kuwasilishwa kwao unachangia katika uradidi wa maudhui ya hadithi. Kwa hivyo visa vinavyonpotiwa na Dzombo vinachangia maudhui ya unyonyaji, ubinafsi, ulaghai na udanganyifu pamoja na yale ya shena kandamizi zilizotungwa na koo mbalimbali za Wachuna kuhakikisha kuwa walijiweka katika hali nafuu kuwakandamiza maskini wazalendo.

Mbali na Dzombo kuwasilisha fikira za Wachuna katika visa hivyo mbalimbali kwa kutumia usemi wa taarifa, pia kuna msimulizi wa nafsi ya tatu ambaye yupo nje ya hadithi na unatusimulia matukio yote hadithini kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi isipokuwa ile sehemu inayohusu utafiti wa Dzombo nchini Walenisi.

Msimulizi huyo, anawasilisha fikira za wahusika wote hadithini kwa kutumia usemi wa taarifa. Kwa mfano anamfuata Dzombo kama mhusika mkuu na kunpoti fikira zake popote aendapo na vilevile kunpoti fikira za wahusika wengine anaokutana nao. Tunaona fikira za mnyongaji 'halali' unapomtia Dzombo sayarini. Vivyo hivyo, fikira za jamaa ya Dzombo, watu wengine na hata Dzombo mwenyewe zimewasilishwa kwetu (hadhira) katika usemi wa taarifa.

Kadhalika, fikira taarifa za Dzombo, ndugu yake, mwajiri wao na karani wa kilimo pia zimewasilishwa kwa usemi wa taarifa. Fikira za mwajiri wa akina Dzombo na karani wa kilimo zinaradidi maudhui ya unyonyaji, umaskini, ukatili, ukoloni mamboleo na ukengeushi

Dzombo anapotua Walenisi, msimulizi anamfuata kwa makini na kuripoti kwa usemi wa taarifa yote yaliyojiri huko Walenisi. Jinsi Dzombo alivyoajabia mandhari ya Walenisi kiasi cha kupachukulia kuwa ni mbinguni imeripotiwa kwa usemi wa taarifa na hivyo ni fikira taarifa za Dzombo. Kwa muhtasari hali inakuwa hivyo katika maingiliano yote ya Dzombo na wenyeji wake huko Walenisi. Hali hii ya uwasilishaji wa fikira inafanana na aina nyingine inayojulikana kama ripoti simulizi ya vitendo vya fikira ambapo fikira zinaonyeshwa kwa matumizi ya usemi wa taarifa lakini kwa kuunganisha taarifa ya ujumbe uliopo kwa kishazi huru kwa kunominisha kishazi arifiwa. Kwa mfano katika ukurasa wa 217, Mtu – Binti Fikirini, anamwambia Dzombo kuwa:

“Walenisi wote kwa jumla, watafirahishwa sana na ushindi huu wake.”

Kwa kuzingatia mfano huu, tunaona kuwa tofauti ya pekee iliyoko baina ya fikira taarifa na fikira simulizi ni kuwa taarifa inaunganishwa kwa kishazi huru kwa kunominisha kishazi arifu. Kwa mfano unominishaji upo kwa nomino ‘ushindi’ badala ya kitenzi ‘shinda’. Hivyo basi tunaweza kudai kuwa fikira za aina hii zinakwendana na usimulizi maizi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi ana sifa za kiungu za kuweza kujua fikira za wahusika kama ilivyo katika *Walenisi*.

Kutokana na mifano hii imebanika wazi kuwa njia za kuwasilisha fikira sawa na zile za unenaji zinaweza kutofautishwa kwa kutumia sifa za kisarufi, kileksika na kiothografia. Sifa za kisarufi ambazo zinaweza kutumika kubaini tofauti hii ni pamoja na alama za uakifishi kama vile kiulizio na alama za mtajo ili kuonyesha unenaji ni wa aina gani na vilevile fikira ni za aina ipi.

Njeo ya vitenzi na viwakilishi nafsi pia hutumika kubaini aina ya unenaji na fikira ambazo zimewasilishwa katika hadithi. Ikiwa viwakilishi nafsi ya kwanza na njeo ya sasa vimetumika, basi tunajua kuwa usemi halisi umetumika na hivyo fikira halisi za moja kwa moja zimewasilishwa. Viwakilishi vya nafsi ya tatu na njeo ya wakati uliopita vinatumika kuwasilisha usemi wa tanfa na hivyo kuwasilisha fikira za taarifa ama ni simulizi au huru kama tulivyoona hapo awali

Mkangi anaturuhusu kuona fikira za wahusika wake kwa kutukaribisha kuona vitu na matukio kwa mtazamo wa wahusika hao, hali ambayo inakwendana na mtazamo wa ndani. Anapobadilisha njia za uwasilishaji wa fikira kuelekea mfumo huru halisi, huwa anatutolea fikira halisi moja kwa moja bila yeye kuingilia kati jinsi alivyofanya wakati ndugu yake Dzombo akizungumza na mwajiri wake. Hali sawa na hii inatokea sehemu mbalimbali katika riwaya wahusika wanaposawirwa katika mazungumzo ya moja kwa moja, kama vile Dzombo na karani wa kilimo, Dzombo na wanyepi wake nchini Walenisi, Dzombo na maskini Jeuri huko kwao Duniani na hatimaye na Mtu-Binti. Fikirini mwishoni mwa riwaya.

Ni wazi kuwa, katika riwaya zilizosimuliwa katika nafsi ya kwanza (ambapo mwandishi anatupa matukio yote kwa mtazamo wa mhusika) kiwakilishi cha nafsi ya kwanza kinaweza kutokea katika fikira taarifa zilizo huru kwa sababu ni sawa katika hali halisi na taarifa iliyonpotiwa kama tulivyoonyesha hapo awali

Tunaweza kuhitimisha sehemu hii kwa kusema kuwa, mwandishi anapowasilisha fikira za mhusika kwa njia yoyote ile huwa anatukaribisha kuona vitu na matukio kwa mtazamo wa mhusika huyo. Kwa mfano tunaona jamii ya Wachuna an Uchuna kutoka kwa mtazamo wa Dzombo. Hata hivyo kuna uwezekano wa kuona vitu kwa mtazamo wa mhusika bila kuwasilisha fikira zake. Kwa mfano katika ukurasa wa kwanza tunaambiwa kuwa Dzombo hakutazamia furuma yoyote kutoka kwa hakimu, kumaanisha kuwa Dzombo tayari alielewa mfumo wa utawala kuwa haukuzingatia haki

Kwa hivyo mtazamo wa mhusika unaweza kuwasilishwa bila kuelezea fikira za mhusika huyo na badala yake mwandishi huelezea vituko mbalimbali kwa njia ambayo vingekonekana kwa mhusika huyo

Aina hizi mbalimbali za uwasilishaji wa fikira zilatumwa na Mkangi kwa sababu anuwai. Kwanza kwa kuonyesha kuwa njia ya kusawiri fikira za mhusika lazima ihusishwe na kuwepo kwa msimulizi maizi. Sababu yenyewe ya kufanya hivyo ni kuonyesha vile njia za uwasilishaji wa fikira zinavyozidi kuchukua thamani tofauti na njia za unenaji. Sharti ikumbukwe kuwa anachosema mhusika ni picha mwafaka ya kile anachofikira.

Hali hii inadhahirika katika hadithi hii kila tunaposimuliwa yaliyosemwa na kutendwa na wahusika mbalimbali ambayo kwa hakika ni matendo yao kwa upande mmoja na fikira zao kwa upande mwingine. Kwa mfano tunaposimuliwa kisa cha maskini Jeuri, tunaona vile Dzombo anavyochukulia matamshi ya maskini Jeuri kijuujuu na kufikira kuwa 'kuwasha taa' ni kuwasha taa kwa hakika ilhali kulingana na maskini Jeuri, kuwasha taa ni kulewa kwa maskini ili kujisahaulisha matatizo ya maisha.

Kadhalika Mkangi aliwasilisha unenaji kwa kutumia usemi halisi au usemi halisi ulio huru ili kutuonyesha vile wahusika wanavyoongea hivi kwamba ungekuwepo ungewaona na kuwasikia bila kuingiliwa na sauti ya mwandishi. Mifano ya kudhahirisha hali hii katika *Walenisi* ni pamoja na wale watu wanaoongea na kutoa maoni yao kuhusu Dzombo baada ya sayari kufyatuliwa katika ukurasa wa sita. Kadhalika, nduguye Dzombo na Dzombo mwenyewe wanapoongea na mwajiri wao, wanafanya hivi katika usemi halisi. Vivyo hivyo Dzombo amesawiriwa katika mazungumzo katika sehemu mbalimbali akiwa huko *Walenisi*.

Kuingilia kati ya mazungumzo kwa mwandishi (sauti ya msimulizi) kunapozidi kupungua, matokeo yake ni uzungumzi nafsia ambapo mhusika hujizungumzia, kama anavyofanya Dzombo katika sehemu mbalimbali za hadithi hii. Sifa za Fikira halisi huru zinapotumika huonyesha kiwango cha udhibiti wa fikira kwa upande wa mhusika yaani ni vipi aseme na ni vipi asiseme kulingana na anavyofikira

Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kuwa, matumizi mwafaka ya uwasilishaji wa unenaji na fikira ni njia mojawapo ya kubadili msimamo, kiimbo na masafa. Jambo hili linamaanisha kuwa mwandishi anapobadili kutoka usemi halisi hadi usemi wa taarifa huwa kimsingi amerefusha masafa kati ya anayezungumza na kinachozungumziwa kama tulivyosema hapo awali. Kulingana na Leech na Short (1981:348):

"kama vile vioo vinavyotoa picha mbalimbali ndivyo diskosi nayo inaweza kuwa na wasimulizi mbalimbali wa simulizi."

Jambo hili linamaanisha kuwa mwandishi ana uwezo wa kuonyesha na kutumia mitazamo mbalimbali katika tukio moja. Kwa mfano msimulizi maizi wa nafsi ta tatu anaelewa nchi ya Walenisi tofauti na jinsi Dzombo anavyoielewa.

Kulingana na Dzombo, Walenisi ni mbinguni lakini kwa msimulizi, Walenisi ni nchi kielelezo ambayo kwayo, Dunia anatokoka Dzombo inalinganishwa. Kwa hivyo kubadili mbinu za unenaji na uwasilishaji wa fikira kunapelekea kubadilika kwa mitazamo ambayo kwayo vitu na matukio mbalimbali yanaangaliwa na kuhukumiwa

SURA YA NNE

WAKATI

Kimsingi, wakati ni muhimu katika maisha ya binadamu. Hata hivyo, dhana hii ya wakati ni changamano kiasi kuwa ni vigumu kuifasili. Sababu yenyewe ni kwamba inahusika na ulimwengu asili pamoja na utambuzi wa binadamu kuhusu ulimwengu huu. Kadhalika, utambuzi wetu unatofautiana kuhusu dhana ya wakati. Kwa mfano, utambuzi wa wakati katika nyakati za enzi ya kati ni tofauti na vile tunavyoelewa sisi (leo) kwa sababu ya jinsi kazi ilivyoamriwa na mabadiliko katika misimu tofauti.

Utambuzi wetu siku hizi umeathiriwa na kubadilishwa na mabadiliko katika sayansi, teknolojia na vyombo vya habari. Fasihi hushughulika na mabadiliko haya inapohusisha dhana ya wakati kama sehemu ya maudhui yake katika matini za kifasihi.

Sura hii itashughulikia wakati na vipengele vyake mbalimbali na jinsi vinavyodhihirika katika hadithi ya *Walensisi*. Kwa vile dhana ya wakati inahusishwa na ulimwengu asili pamoja na utambuzi wetu kuhusu ulimwengu, hivyo basi dhana hii inahusishwa na mwanda matini, yaani ule ulimwengu bunilizi ambao unawasilishwa katika matini simulizi.

Lakini katika sura hii tutaangazia zaidi wakati katika simulizi kuliko mwanda wa simulizi. Sababu yake ni kwamba nadharia ya naratolojia imebuni na kustawisha mbinu za kufafanua wakati kuliko mwando matini.

Inahalisi kusema kuwa, wakati ni dhana ambayo inaandikiwa na waandishi na pia ni kipengee katika hadithi na diskosi, kwa hivyo tunaweza kusema kuwa wakati katika simulizi ni uhusiano wa kronolojia kati ya hadithi na matini yaani jinsi matukio yanavyohusiana katika kutendeka kwao moja baada ya jingine.

Matukio yoyote hutendeka katika wakati fulani. Uhakiki wa kina-naratolojia umezua anuwai mbili za dhana ya wakati. Kuna wakati inaochukua hadithi-hadithi na wakati-matini, ambapo wakati hadithi hurejelea wakati inaochukua hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho wake. Wakati huu unaweza kuwa siku moja, mwaka mmoja au hata kame nyingi. Kwa mfano, hadithi ya *Walenisi* imechukua muda mrefu tangu Dzombo kuteswa na kunyanyaswa akiwa mfanyikazi, kisha mkulima na baadaye kuhukumwa kifo kwa sayari.

Ilimchukua Dzombo miaka miwili tangu ahukumwe kifo hadi atue nchini Walenisi. Katika ukurasa 34, tunasoma:

"Alipepesuka alipokanyaga ardhini, kwani miguu yake haikuwa imetembea kwa zaidi ya miaka miwili."

Kadhalika, ilimchukua miaka mingine miwili akifanya utafiti katika maktaba ya kitaifa nchini Walenisi. Katika ukurasa 152, tunasoma,

"Aliufanya utafiti huu kwa muda wa miaka miwili (mwaka mmoja wa kiwalenisi ikiwa miaka mitano ya Duniani), na baada ya kuchambua kwa muda huu wote ndipo alipoamua kuandika mswada. . ."

Katika mswada huo, Dzombo ananpoti visa na matukio mbalimbali katika enzi ya Uchuna ambayo yalifanyika kwa muda mrefu kabla ya wawalenisi kutambua uovu wa utawala wa Uchuna na kuungana pamoja ili kuondoa hali hiyo. Kwa mfano, katika ukurasa wa 168, Dzombo anasema

"miaka nenda miaka rudi, koo za wachuna zikawa zimejipamua vilivyo".

Kimsingi tunaweza kusema kuwa wakati-hadithi katika hadithi ya *Walenisi* ni mrefu kiasi cha kutokadirika kikamilifu kwa jinsi ambavyo umefumbata enzi mbili tofauti. Kuna enzi ya Wachuna na Uchuna ambayo ilichukua miaka na mikaka na vile vile kuna enzi baada ya Uchuna, yaani Uwalenisi ambayo pia imesimuliwa kuwa imechukua muda mrefu kiasi cha kupata maendeleo yanayosimuliwa.

Kwa upande mwingine, wakati-matini ni wakati msomaji anaweza kuchukua kusoma matini fulani. (Lothe:54) Shida ni kuwa hakuna njia inayoweza kutumika kutathimini au kupima wakati-matini. Hata hivyo, kigezo ambacho kinatumiwa lakini bila mafanikio makubwa ni muda anaohukua msomaji kusoma hadithi husika. Kigezo hiki si mwafaka kwa jinsi ambavyo wasomaji wana kasi tofauti za usomaji.

Ili kuzifahamu dhana za wakati-hadithi na wakati-matini, tutaangalia mfano wa Dzombo akiwa sayarini na anaporudisha fikira zake nyuma na kuangazia yaliyomsibu katika nchi yake na aliyoyafanya hadi kuhukumwa kifo kwa sayari (ukurusa 14-21). Katika kurasa hizi, kuna kipindi kirefu ambapo Dzombo hafanyi lolote isipokuwa kufikina yaliyompata akiwa Duniani (Dzombo hafanyi lolote) ilhali wakati-matini ni mrefu (msomaji anaendelea kusoma).

Dzombo akiwa sayarini na *Walenisi*, anasawiriwa akiyakumbukia matukio yaliyofanyika awali. Anapofanya hivi huwa hachangii hadithi kimbele na hivyo wakati-hadithi unabakia nunge au unakuwa mfupi ukilinganishwa na wakati-matini ambapo msomaji anaendelea kusoma. Visa vinavyodhihirisha hali hii ni pamoja na kile cha mzee Matigasi katika (uk.90), kisa cha Maskini Jeuri katika (uk.68), na kile cha Dzombo kukumbuka mkeweae Hani katika (uk.126) miongoni mwa visa vingine.

Genette, katika *Narrative Discourse*, anahusisha wakati-hadithi na vipengee vitatu muhimu. Navyo ni pamoja na mpangilio, muda na idadi marudio. Tunapozungumzia mpangilio tunamaanisha mfuatano wa matukio katika hadithi kulingana na uwasilishaji wake katika simulizi. Jambo hili linamaanisha kuwa matukio katika hadithi yanaweza

kusimuliwa kulingana na kutokea kwao kiwakati. Hali ikiwa hivyo, basi msuko wa hadithi na mpangilio hulingana.

Kadhalika ikiwa hadithi imesimuliwa kwa namna ambayo inakiuka ule mpangilio wa kronolojia wa hadithi, basi hapo hutokoa tofauti ambayo inaelezwa kama anakroni ambayo kulingana na Wamitila akimunukuu Mieke Bal (2003:23)anasema.

*“ukosefu wa mapatano kati ya jinsi
matukio yanavyoonekana katika msuko na
jinsi yanavyopatikana katika hadithi”*

Hivi ni kusema kwamba hadithi inasimuliwa kwa kutumia viona nyuma (virejeshi) na viona mbele (vielekezi mbele) mtawalia.

Viona nyuma hutumika kusimulia matukio katika hadithi wakati ambapo matukio ya nyuma yamesimuliwa. Hivi ni kusema kuwa usimulizi unaruka na kwenda katika mahali pa awali au mbeleni, yaani matukio yaliyopita yanafumbatwa katika mbinu hii.

Kabla ya kutoa mifano inayoakisi kudhihirika kwa hali hii katika *Walenisi*, inahalisi tufafanue ni kwa nini waandishi hutumia viona nyuma. Sababu mojawapo ni kuwa mbinu hii hutoa msingi wa matukio ya wakati uliopo. Kwa mfano, katika kurasa za 12-21, Dzombo akiwa sayanni baada ya kuhukumiwa kifo, anakumbuka hali ilivyokuwa kabla ya kuhukumiwa kifo, kumaanisha kuwa matukio yaliyotokea kabla ya hukumu ya kifo yanafumbatwa ili kueleza sababu za hukumu hiyo kali

Vile vile npoti ya utafiti wa Dzombo inaakisi matumizi ya viona nyuma. Katika utafiti, msimulizi anaturudisha nyuma hadi enzi ya Uchuna, kama njia ya kueleza hali iliyoko katika Dunia anakotoka Dzombo. Watu wa Duniani wana unafiki, ufidadi, wizi, ulaghai na maovu mengine mengi kwa sababu ya kukolezwa au kurithi tabia hiyo ambayo ni ya kichuna.

Sababu nyingine ya kutumia viona nyuma ni kuwapa wahusika msingi wa kuonyesha sababu za matendo yao fulani. Katika ukurasa wa 21, Dzombo anakumbuka kisa chake na karani wa kilimo na kuonyesha sababu yake ya kuazimia kuwa mwanaharakati. Katika ukurasa huo tunasoma:

*"Dzombo aluchwa pale ndani akikodolea macho meza
iliyokuwa imejaa makaratasi. Alifungua kigunya chake
na akatazama kile kikatasi. Haikuwa karatasi tena hali
pingu zilizokirwa zikimfyanda kutoka utosini hadi
nyayoni. Kwa hasira nyingi, alikutupa chini na
kukisaga kwa kisigino na akatoka nje. Ndipo hapo
alipokata shauri kwenda kusoma angalau aweze
kuelewa utandu huu wa ujinga"*

Kwa kutumia mbinu hii inaeleweka kuwa Dzombo alikuwa mwanaharakati kwa kuchochewa na hali ya shuruti kutoka kwa karani wa kilimo. Tabia hii ya uanaharakati ilipelekea kufutwa kwake kazi na baadaye kushtakiwa kwa kuwachochea wafanyikazi watifu.

Kadhalika, Dzombo akiwa *Walenisi* akifurahia jinsi alivyolakiwa kwa vinywaji na vyakula, alikumbuka kisa alichokishuhudia kwa mzee Matigusi wakawa pamoja na Maskini Jeuri. Kutokana na umaskini uliokolea Duniani, watu hawakuweza kununua pombe na vinywaji vingine halali na badala yake waliazimia kunywa chang'aa angalau wajipumbaze na kusahau umaskini wao. Lakini kule Walenisi hali ilikuwa tofauti kwa sababu ya msingi thabiti wa uchumi uliohakikisha kuwepo kwa usawa, hali ambayo inafafanua ni kwa nini wawalenisi walitofautiana kitabia na watu wa Duniani.

Vile vile, Dzombo anamkumbuka mkewe na watoto wake watano. Kisa hiki ni ishara kuwa Dzombo ameanza kubadilika na kuwa na tabia ya utu ambayo ni matokeo ya safani ya utu akiwa *Walenisi*. Vile vile ni ishara ya kuona haya kwa jinsi ambavyo alikuwa na hisia kali za kimapenzi kwa Mtu-Binti Fikirini. Katika ukurasa wa 126, tunasoma:

*“kwa ghafla, akaruka mpaka Duniani kwa mkewe
Hani na watoto wao watano: wavulana watatu na
wasichana wawili. Maskini Hani, mkewe alikuwa
mjane sasa! Maisha hayakuwa mapesi kabla ya kifo
chake, sembuse hivi sasa?”*

Kwa kutilia mkazo hoja kwamba Dzombo amepita hatua mbalimbali za ubadilikaji tabia na kuwa mtu, tunaona ni vipi anakumbuka maisha ya watu wa Duniani, kwa hisia za huruma nyingi. Katika ukurasa wa 216, tunasoma:

*“Ukweli ni kwamba, ufahamu wa kiutu umenifanya
kiwafikira wenzangu huku Jehanamu vile
wateswavyo, wanyanyaswavyo, waumizwavyo,
wapumbazwavyo na kwa jumla kuishi katika hali
ya uzima-mauti ya ukweli-uongo wanaopewa na
Wachuna wa huko. . . ni fikira hizi ndizo zinazonitia
simanzi sana mara kwa mara . . .”*

Dzombo anawakumbuka watu wa Duniani kwa sababu moja kuu. Sababu yenyewe ni kuwa sasa amebadilika na kuwa kiumbe kipya, labda azimio la mwandishi la kujenga jamii mpya huenda likafanikiwa Dzombo atakaporejea Duniani akiwa na mtazamo tofauti kuhusu mambo mbalimbali ya kifalsafa na kijamii. Ni muhimu tukumbuke kuwa sababu mojawapo ya kutumia viona nyuma ni kuwapa wahusika msingi wa kuonyesha sababu za matendo fulani wanayoyatenda kama tulivyosema hapo awali

Sababu nyingine ya kutumia viona nyuma ni kutoa maelezo muhimu ya kuikamilisha hali fulani, kwa kuhusisha matukio mbalimbali. Mfano mwafaka wa kumulika hali ni vile visa vya mapacha, moto, mabavu na cha mchawi. Visa hivi vinaturudisha nyuma katika enzi ya Uchuna na kufafanua jinsi mban/koo tofauti za Uchuna zilivyoanza na ni kwa nini hali ya maisha iko jinsi ilivyo Duniani alikotoka Dzombo

Hali kadhalika, kwa kuangazia visa hivi, tunaweza kufahamu (kiulinganuzi) ni kwa nini Walenisi ikafikia hali yake ya sasa kimaendeleo huku Dunia ikibakia nyuma. Vivyo hivyo visa hivi vinamkuza Dzombo kama mwanaharakati aliyeimanka zaidi na hivyo kuendeleza mapambano dhidi ya Uchuna atakaporudi Duniani.

Viona mbele (vielekezi) kwa upande mwingine husimulia matukio yajayo au huelekeza kwa matukio hayo. Hivi ni kumaanisha kuwa ni ruteka inayohusisha kuleta mapema matukio yatakayotokea baadaye katika hadithi. Kadhalika mbinu hii ya anakroni inahusisha hali inayoonyesha ukiushi kutoka kwa hadithi kuu. Kwa ufupi viona mbele ni kuleta matukio ya baadaye katika hadithi kabla ya matukio ya sasa kusimuliwa.

Ni nadra mbinu hii kutokea katika hadithi ikilinganishwa na mbinu ya viona nyuma. Hata hivyo, katika hadithi ya *Walenisi*, viona mbele vimetumika wakati Dzombo anaposawiriwa katika ndoto. Katika ukurasa wa 49, Dzombo anaota kuhusu Mtu-Binti Fikinini. Vivyo hivyo katika kurasa za 133-137, pia anaota (Dzombo) kuhusu msichana huyo. Ndoto hizi mbili ni kama ubashiri wa mapenzi na baadaye ndoa kati ya Dzombo na Binti-Fikinini. Mapenzi na ndoa kati ya wawili hawa ni tukio lililotokea baadaye katika hadithi, lakini limesimuliwa kabla ya kutokea kwake kupitia ndoto.

Kipengee cha pili kinachofumbata dhana ya wakati katika hadithi ni muda. Swali la kujuliza ni je, tukio limechukua muda mrefu au mfupi? Ni vigumu kujibu swali hili. Kigezo cha pekee tunachoweza kutumia ni muda anaoweza kuchukua mtu fulani kusoma hadithi fulani. Hata hivyo, wasomaji tofauti wana kasi tofauti za kusoma.

Kuna hali ambapo wakati-hadithi na wakati-matini huwa sawa, yaani katika onyesho sababu ya jambo hili kutokea ni kwamba, dayolojia katika onyesho huwasilisha lugha katika lugha tukizingatia kuwa maneno katika matini huwasilisha maneno yaliyotamkwa katika hadithi kama tutakavyoona hivi punde.

Kwa vile ni vigumu kukadiria mpito wa wakati, Genette (1980) na pia Kenan (1983), walipendekeza mkabala unaounganisha mshabaha wa wakati-matini na mwanda-matini, ambapo hadithi inaweza kuchukua muda mrefu (unaweza kuwa dakika chache au miaka mingi) unaohusiana na kiasi cha wakati wa kuwasilisha hadithi.

Urefu wa matini, ambao ni sehemu ya mbinu ya usimulizi ya mwandishi, una umuhimu kwa kipengee cha wakati-matini. Genette anapendekeza kutumia kile anachokuita kasi au spidi thabiti kama kigezo cha kupimia viwango mbalimbali vya mpito wa wakati Spidi thabiti inamaanisha

“uwiano kati ya muda unaochukuliwa na hadithi na vipi matini inabakia thabiti bila kubadilika Kwa mfano riwaya inaweza kutumia kila ukurasa mmoja kuwasilisha mwaka mmoja katika maisha ya mhusika fulani” (Lothe 2000: 57).

Kwa kutegemea kigezo hiki, kasi ya wakati inaweza kuongezeka au kupunguka. Kasi ya juu ni udondoshi na kasi ya chini ni mtuo. Kati ya kasi ya juu na ya chini kuna muhtasari na onyesho. Kufikia hapa, tunaweza kusema kuwa muda kama kipengee cha wakati unadhihirika kwa jinsi nne tofauti, yaani udondoshi, mtuo, muhtasari na onyesho. Swali ni je, jinsi hizi zinadhihirika vipi katika hadithi ya *Walenisi*?

Tukianza na mtuo, utapata kwamba kuna wakati-matini mrefu na wakati-hadithi mfupi au nunge. Mifano mizuri ya hali hii katika *Walenisi* ni katika kurasa za 32-33 ambapo kuna sauti za kuogofya sayani. Hapa wakati-matini ni mrefu lakini wakati-hadithi ni nunge.

Mifano yote inayoakis mbinu rejeshi vile vile inaweza kutumika katika hali hii. Sababu yenyewe ni kwamba, mbinu rejeshi haipeleki hadithi kimbele bali inaongeza wakati-matini (msomaji azidi kusoma) inapotumika. Kadhalika Dzombo anapoota ni mfano mwingine wa mtuo kwa vile amelala na kuota bila kutenda lolote.

Vile vile muhtasari ni jinsi nyingine ambayo kwayo muda hudhahirika kama kipengee cha dhana ya wakati katika hadithi. Katika muhtasari, wakati-matini ni mfupi kuliko wakati-hadithi. Pamoja na onyesho muhtasari hutumika sana katika simulizi bunifuzi na aghalabu huunganishwa Kenan (1983:53) anasema:

*"kasi ya hadithi huharakishwa katika muhtasari,
hili linatokana na ufupishwaji wa muda fulani
wa hadithi kwa kauli chake"*.

Katika ukurasa wa 100 wa hadithi ya *Walenisi*, tunasoma:

*"Lakini ni katika karne mbili tu zilizopita, hasa baada
ya kuubumburusha utawala wa wachuna, ndipo
ilipoweze kana wataalamu kuutafiti kwa dhati
na kuutumia ipasavyo kwa manufaa ya kila mmoja wetu"*.

Dondoo hilo hapo juu ni fupi, lakini wakati hadithi unaorejelewa ni mrefu sana, yaani karne mbili.

Mfano wa pili wa muhtasari ni katika ukurasa wa 152, ambapo tunasoma:

*"Aliufanya utafiti huu kwa muda wa miaka miwili
(mwaka mmoja wa kiwalenisi ikiwa miaka
mitano Duniani) na ni baada ya kuchambua kwa
muda wote ndipo alipoamua kujiandikia mswada."*

Mifano ya muhtasari ni mingi sana kama vile kurasa za 11, 24, 33, 34, 51, 53, 74, 96, 146, 148, 168, 174, 192 na kadhalika

Muda vile vile hudhahirika katika onyesho ambapo wakati-matini ni sawa na wakati-hadithi. Kuna mambo mawili muhimu ya kukumbuka kuhusu wakati-matini kwanza (kama tulivyoona hapo awali) ni kuwa wakati-matini hulingana na wakati-hadithi. Pili,

onyesho pia husimuliwa. Hali hii hutumika katika matini ambazo mwandishi aghalabu hutumia dayolojia. Kenan (1983:54) anasema:

*“Inapotegea dayolojia pekee pamoja na kiasi kidogo
cha maagizo ya jukwaa taarifa huonekana
kama onyesho kutoka tamthilia kuliko sehemu ya simulizi”.*

Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa hali hii inaleta sifa ya uigizaji katika matini ambapo wahusika wanasawiriwa wakiwa wanazungumza mbele ya wasomaji wa kazi hiyo ambapo mchango wa msimulizi wa nafsi ya tatu ni mdogo, ingawa tunagundua kuwepo kwake katika kauli arifu. Kwa mfano kunapotokea ubishi baina ya karani wa kilimo na Dzombo, tunaona msimulizi akiingilia kati kwa kutoa kauli arifu kuwa:

‘karani akamkubalia’ (19).

Hali hii inadhihinka pakubwa katika nwaya ya *Walenisi*, tunapowaona wahusika mbalimbali wakiwa katika mazungumzo. Mifano ya maonyesho ni pamoja na wale watu waliofadhaishwa na hukumu dhidi ya Dzombo, mwajiri na nduguye Dzombo kwa upande mmoja na Dzombo na mwajiri kwa upande mwingine. Kadhalika Dzombo anasawiriwa akiwa katika mazungumzo na karani wa kilimo na vilevile na Maskini Jeuri wakiwa kwa mzee Matigasi pamoja na walevi wengine. Mazungumzo pia yanadhihinka baina ya Dzombo na wenyeji wake akiwa nchini Walenisi.

Matumizi mapana ya maonyesho hupelekea (ingawa si lazima) kuwa na matini ndefu. Dayolojia huonyesha uamilifu shadidi na wa kidrama ambao onyesho huwa nayo. Athari kubwa ya onyesho hujikita katika jinsi matini imeunganishwa na jinsi dayolojia inahusishwa na maoni ya msimulizi.

Msimulizi wa nafsi ya tatu huwa anaarifu kuliko kuelezea na hivyo kuchangia na kuimarisha muumano wa simulizi. Jambo hili linamaanisha kuwa anawaacha wahusika wazungumze halafu baadaye anatoa kauli arifu kama inavyodhihinka katika sehemu mbalimbali kunako mazungumzo.

Mbali na onyesho, jinsi nyingine ambayo kwayo muda hudhahirika inajulikana kama udondoshi ambapo tunapata kuwa kwa wakati-hadithi fulani, kuna mwanda nunge wa kimatini Jambo hili linamaanisha kuwa wakati-hadithi ni mrefu ilhali wakati-matini ni nunge. Hali hii hudhahirika kwa njia mbili.

Kwanza kabisa kuna udondoshi wazi ambapo matini huonyesha dhahiri kiasi cha muda ambao umepita au umerukwa katika simulizi, ndivyo kusema kuwa musimulizi anataja muda ambao umepita, iwe ni siku moja, mwezi, miaka na kadalika. Kwa mfano katika ukurasa wa 7, tunasoma:

*"mle kaburini alimokuwa, hakupoteza wakati
Alikuwa ameshaamua dakika tano ni nyingi
sana kwa mtu kufufuka, sembuse kwa mtu kufa.."*

Katika dondoo hilo, msimulizi ameonyesha bayana kiasi cha muda ambao ungepita ili mafuta katika mitambo ya sayari kuisha na hivyo Dzombo kuangamia. Hali ikiwa hivyo tunasema kuwa huo ni udondoshi ulio dhahiri.

Katika ukurasa wa 34, tumeanfiwa kuwa kabla ya kutua Walenisi, miguu yake Dzombo haikuwa imetembea kwa zaidi ya miaka miwili. Kwa hivyo, kutokana na maelezo haya tunaelewa kuwa Dzombo alichukua muda wa zaidi ya miaka miwili akiwa safarni kwa sayari. Hata hivyo, mwandishi anajikinza kwa sababu hapo awali kabla ya Dzombo kuingizwa kwenye sayari tulianfiwa kuwa mafuta mitamboni mwa sayari yangechukua muda wa dakika tano pekee.

Mfano mwingine wa udondoshi ni ule unaopatikana katika ukurasa wa 51 ambapo tunasoma:

*"Trimi zenyewe zilikuwa zikienda mwendo wa kasi
zaidi ya upepo wa kimbunga. Safari ilikuwa ya*

*siku kumi. Lakini ingekuwa ya miaka kumi
kama wangesafiri kwa sayari yake.*

Kutokana na mfano huu, tunaelewa ni muda gani Dzombo na wenzake walichukua walipofunga safani ya kupima utu wake Dzombo. Mifano zaidi ya aina hii ya udondoshi ni katika kurasa za 152, 164 na 171 miongoni mwa nyingine.

Udondoshi usio wazi kwa upande wake ni hali ambapo utakuta kwamba hakuna wakati dhahiri unaotajwa ili kurejelea mabadiliko katika wakati-hadithi, yaani hatujui kilichoachwa nje au ni kiasi gani cha muda usimulizi umeruka. Katika ukurasa wa 21, tunasoma

*"Kwa hasira nyingi, alikitupa chini na kukusaga kwa
kisigino na akatoka nje. Ndipo hapo alipokata shauri
kwenda kusoma ili angalau aweze kuelewa utandu
huu wa ujinga."*

Katika mfano huu, hakuna wakati dhahiri ambao umetajwa kuonyesha kiasi cha muda Dzombo alienda masomoni na vile vile ile sehemu ya masomo yake imedondoshwa katika usimulizi.

Kadhalika katika kile kisa cha mapacha, kuna sehemu inayodhihirisha udondoshi usiowazi. Katika sehemu hii, tunapata kuwa mwanaye Chihenyoo kwa jina la Mefuraha alisoma na kuhitimu na baadaye kuwa daktari. Lakini hatumwoni akiwa shuleni akisomea taaluma ya utabibu na vile vile hatumwoni akifanya kazi hiyo. Muda aliochukua shuleni pamoja na maisha yake shuleni vimedondoshwa.

Udondoshi unapotumika katika usimulizi, huleta athari ya taharuki inayomchochea msomaji kuendelea kusoma zaidi ili kuelewa au kuona kinachotokea baadaye katika maisha ya mhusika anayesawiriwa katika hali hiyo na hivyo matarajio yake kujibiwa na kupata au asipate mliwazo.

Kipengee kingine ambacho kinadhibitisha dhana ya wakati katika hadithi ni umara au idadi marudio. Kwa maoni ya Lothe(2000:60) idadi marudio:

*“Hurejelea uhusiano kati ya mara ngapi tukio
fulani lilitendeka katika hadithi na ni mara ngapi
tukio hilo limesimuliwa au kutajwa katika
matini.”*

Hivyo basi idadi marudio huhusisha kurudiarudia ambako kwenyewe ni dhana muhimu ya kisimulizi. Ni muhimu kukumbuka kuwa si lazima miundo ya kileksika na kisintaksia ishabihiane tukio linaposimuliwa mara kadhaa. Uhusiano kati ya matukio hadithini na usimulizi wao katika matini hudhahirika kwa njia tatu muhimu

Tukio lililofanyika mara moja kusimuliwa mara moja. Huu ndio mfumo wa idadi marudio uliozoeleka na hali hii inadhibitika pakubwa katika hadithi ya *Walenisi*. Tukio la kutiwa mbaroni na kuhukumiwa kifo limetokea mara moja na limesimuliwa mara moja, yaani Dzombo hajasimuliwa tena akiwa kotini.

Baada ya Dzombo kuhukumiwa kifo, kuna watu wanaotajwa kuwa ni wafadhaishwa, ambao wametokezwa mara moja tu katika hadithi hii na walilofanya ni kufadhaika na pia kumcheka Dzombo na kujiona kuwa wenye bahati kwa vile hawajashikwa na kuhukumiwa. Tukio hili limefanyika na kusimuliwa mara moja

Tukio la Dzombo kukumbana na majabali katika anga za mbali limesimuliwa mara moja. Vile vile utafiti wa Dzombo katika maktaba kuu ya *Walenisi* umefanywa na kusimuliwa mara moja. Kwa ujumla kama tulivyotaja hapo awali matukio mengi yametokea na kusimuliwa mara moja kwa sababu kitendo huu ndio umezoeleka.

Kwa upande mwingine, tukio lililofanyika mara moja linasimuliwa mara nyingi hali ambayo inajulikana kama usimulizi ghibu. Hii ni mbinu muhimu katika simulizi za fasihi

za sasa. Hata hivyo kuna mifano ya zamani kama katika *Bibilia* ambapo injili katika *Agano Jipya* ni hadithi moja inayorudiwarudiwa kuhusu maisha ya Yesu Kristo.

Hali hii ya urudaji huleta uchangamano wa kimaudhui kwa sababu tukio linaporudiwa huwa linarudiwa katika muktadha tofauti na miktadha iliyotangulia.

Kama tulivyosema hapo awali ni kuwa tukio linaporudiwa si lazima miundo ya sentisi na maneno sawa itumike

Suala la dhuluma limerudiwa mara kadha katika hadithi ya *Walenisi*, lakini kila linaporudiwa miundo tofauti ya maneno na hata miktadha linapoangazwa hutumika Dzombo anadhulumiwa katika mahakama anaponyimwa nafasi ya kujitetea. Vile vile anadhulumiwa mahindi yake yanapofyekwa kwa madai kuwa aliyapanda bila kazingatia ushauri wa kitaalamu.

Idara ya kilimo na utawala wa Duniani unamdhulumu Dzombo mara nyingine kwa kutomlipa baada ya kuwauzia mazao yake ya kilimo na badala yake kumdar yeye (Dzombo) kwa mbolea aliyochukua kutoka kwa idara hiyo.

Kwa mara nyingine, suala la dhuluma linarudiwa tunaposimuliwa kuhusu mabavu ambaye aliwadhulumu wasichana kwa kuwabikin tu na kuwaacha kwa madai kuwa wazazi wao wangepata ulinzi (k)wake dhidi ya wanyama wakali wa pori.

Vivyo hivyo, dhuluma dhidi ya wanawake inasimuliwa kwa mzee Matigasi Dzombo wakiwa na Maskini Jeun Jambo hili pia linasimuliwa Dzombo anapozungumza na wenyeji wake huko Walenisi. Katika ukurasa wa 135 tunasoma:

*“Kwenu, mwanamke ni embe lililova ukishalila
huwa ni kokwe (kokwe) ya (la) kutipiliwa mbali ...
Kwenu mwanamke ni ndizi: ukishalila huwa ganda
la kutipiliwa (kutupwa) jaani ...”*

Tukio jingine ambalo limerudiwa mara kadhaa ni mapenzi ambapo kuna mapenzi kati ya Dzombo na Mtu-Binti-Fikinni kwa upande mmoja na kati ya Dzombo na mkwewe Hani na watoto wake kwa upande mwingine. Vile vile kuna mapenzi kati ya Kadzo na Dutu ambayo ni ya dhati na pia kati ya mabavu na Kadzo ambayo ni ya kulazimishwa.

Safan ni tukio lingine ambalo limerudiwa si haba. Kwanza kabisa kuna safari inayofanywa na Dzombo iliyodhaniwa kwamba ingempeleka mautini lakini baada ya ujasin mkubwa anatua nchini Walenisi. Alipotua, alifanya safari nyingine kwa trimi kuelekea kwa wenyeji wa nchi hiyo.

Baada ya kulakiwa kwa vyakula na vinywaji, alipumzishwa na kisha kupelekwa kwa safari ya utu ambapo alitarajiwa kupitia hali mbalimbali za kumbadilisha kuwa kiumbe mpya na razini kinyume na wenzake wa kule Duniani.

Baada ya safari ya utu, anapelekwa kwa safari nyingine ambapo alishuhudia miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Kisha alipelekwa kwa safari ya mapenzoni, ambapo aliona na kustaajabia mengi ambayo yalikuwa ndoto huko kwao Duniani.

Safari ya mwisho ni ya Dzombo kurudi kwao Duniani. Hii ni ishara ya hatua ya mwisho katika ubadilikaji wa Dzombo kuwa kiumbe mpya na vilevile kuashina kuanzishwa kwa jamii mpya. Hata hivyo, sehemu hii imedondoshwa na hivyo hatujui Dzombo alipokelewa vipi alipofika kwao. Kama tulivyosema hapo awali, athari mojawapo ya udondoshi ni kuzua taharuki, yaani hatujui watu wa Duniani watafanya nini watakapomwona Dzombo aliyedhaniwa kufa kurejea nyumbani.

Kadhalika umara unajitokeza pale tukio lilolotokea mara kadhaa linasimuliwa mara moja. Katika hali hii, kisimuliwacho ni kilichokuwa kinafanyika. Kwa mfano, katika utafiti wake, Dzombo anaripoti matukio ambayo yalikuwa yakifanyika wakati wa enzi ya Wachuna. Ingawa visa anavyosimulia kuhusu chimbuko la koo mbalimbali za Wachuna vilitokea mara kadha, Dzombo anavitaja (kuvisimulia) mara moja.

Tukio jingine ambalo limerudiwa mara kadhaa ni mapenzi ambapo kuna mapenzi kati ya Dzombo na Mtu-Binti-Fikirini kwa upande mmoja na kati ya Dzombo na mkwewe Hani na watoto wake kwa upande mwingine. Vile vile kuna mapenzi kati ya Kadzo na Dutu ambayo ni ya dhati na pia kati ya mabavu na Kadzo ambayo ni ya kulazimishwa

Safari ni tukio lingine ambalo limerudiwa si haba Kwanza kabisa kuna safari inayofanywa na Dzombo iliyodhaniwa kwamba ingempeleka mautini lakini baada ya ujasiri mkubwa anatumia Walenisi. Alipotua, alifanya safari nyingine kwa trimi kuelekea kwa wenyeji wa nchi hiyo.

Baada ya kulakiwa kwa vyakula na vinywaji, alipumzishwa na kisha kupelekwa kwa safari ya utu ambapo alitarajiwa kupitia hali mbalimbali za kumbadilisha kuwa kiumbe mpya na razini kinyume na wenzake wa kule Duniani.

Baada ya safari ya utu, anapelekwa kwa safari nyingine ambapo alishuhudia miradi mbalimbali ya kimaendeleo Kisha alipelekwa kwa safari ya mapenzi, ambapo aliona na kustaajabia mengi ambayo yalikuwa ndoto huko kwao Duniani.

Safari ya mwisho ni ya Dzombo kurudi kwao Duniani. Hii ni ishara ya hatua ya mwisho katika ubadilikaji wa Dzombo kuwa kiumbe mpya na vilevile kuashina kuanzishwa kwa jamii mpya. Hata hivyo, sehemu hii imedondoshwa na hivyo hatujui Dzombo alipokelewa vipi alipofika kwao. Kama tulivyosema hapo awali, athari mojawapo ya udondoshi ni kuzua taharuki, yaani hatujui watu wa Duniani watafanya nini watakapomwona Dzombo aliyedhaniwa kufa kurejea nyumbani.

Kadhalika umara unajitokeza pale tukio lilolotokea mara kadhaa linasimuliwa mara moja. Katika hali hii, kisimuliwacho ni kilichokuwa kinafanyika. Kwa mfano, katika utafiti wake, Dzombo anaripoti matukio ambayo yalikuwa yakifanyika wakati wa enzi ya Wachuna. Ingawa visa anavyosimulia kuhusu chimbuko la koo mbalimbali za Wachuna vilitokea mara kadha, Dzombo anavitaja (kuvisimulia) mara moja.

Matukio yaliyosimuliwa mara moja ingawa yalitokea mara kwa mara yalifumbatwa katika visa vya mapacha, moto, mabavu na mchawi ambavyo ni muhtasari wa maovu yaliyojin kila siku katika enzi ya Uchuna. Katika ukurasa wa 168, tunasoma:

*“Miaka nenda miaka rudi, koo zu Wachuna zikawa
zimejipamua vilivyo”*

Badala ya kusimulia matukio haya kila mwaka, msimulizi ameyasimulia mara moja kwa kuyafumbuta katika visa hivyo tofauti.

Baada ya maskini kukolezwa kasumba ya kuamini kuwa hali yao ni majaliwa, ndipo wachuna walivyozidi kujiendeleza huku maskini wakiendelea kusongonyoka, hali ambayo iliendelea kwa muda mrefu. Lakini badala ya kusimulia hali hiyo baada ya kila mwaka, msimulizi anaitaja mara moja kwa njia inayotufanya tuelewe kuwa matukio hayo yalijiri siku baada ya siku. Katika ukurasa wa 192, tunasoma:

*Udundu uliwarudisha nyuma na kukosa hata kuona
wapi walikokuwa wakienda. Hali hii ilidumu kwa karne
nyingi kwa sababu walikuwa wamekitwa
upumbavuni kwa kuvikwa figa la unjinga
na werveu wachuna.”*

Jinsi nyingine inayodhihinsha muda kama kipengee cha wakati katika hadithi ni uendelezaji. Dhana hii inahusiana kwa kiasi kikubwa na mtuo. Katika hali hii wakati-matini unaelekea kuwa mrefu kuliko wakati-hadithi ambapo mawazo ya mhusika fulani yanaangazwa hasa kupitia saikolojia yake.

Hali hii inaenda pamoja na usimulizi maizi ambapo msimulizi anaelewa saikolojia na ndoto za wahusika wake. Kati ya ukurasa wa 133 na wa 137, tunaonyeshwa ndoto ya Dzombo akiwa usingizini ambapo anamwota Mtu-Binti-Fikinni pamoja na bibie Hani

Dzombo yu usingizini na hatendi lolote isipokuwa kuota na hivyo wakati-matini ni mrefu (msomaji anaendelea kusoma) ilhali wakati-hadithi ni mfupi (Dzombo hatendi lolote)

Mifano yote ya viona nyuma pia inaweza kuakisi hali hii kwa jinsi ambavyo vinafungamana na saikolojia au fikira bila kuvitoa nje isipokuwa tunaelewa haya kupitia kwa usimulizi maizi. Katika hali hii, wakati-hadithi ni mfupi ukilinganishwa na wakati-matini kwa sababu ambazo tayan zimetajwa na hivyo haviendelezi hadithi mbele kiwakati na kipahali.

Kufikia kiwango hiki, tumeangazia dhana ya wakati na jinsi unavyodhihirika kwa njia mbalimbali katika hadithi ya *Walenisi* na kutoa mifano anuwai inayoakisi vipengee tofauti vya kiwakati. Hata hivyo hadithi hii inadhihirisha dhana ya wakati kwa njia ya kifalsafa, ambapo kuna wakati mwujiza usioeleweka moja kwa moja na wakati halisi ambao unaeleweka lakini unaowakilishwa na wakati mwujiza

Mandhari na maendeleo ya kijabu yanayosimuliwa ni ishara kuwa maendeleo ya kiwango sawa na cha *Walenisi* yanaweza kufikiwa huko Duniani ikiwa watu watahiriki pamoja na kung'oa tabia ya kichuna. Hivi ni kusema kuwa nchi kielelezo (*Walenisi*) ni ya ajabu lakini inaakisi hali halisi kuwa maendeleo yanaweza kupatikana Duniani ikiwa wananchi wa huko (*Duniani*) watajitolea kufanya bidii

Kadhalika historia ya *Walenisi* inaweza kuangaliwa kama mtazamo mpana wa historia ya binadamu pamoja na uzukaji na uendelezaji wa mifumo tofauti ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ili kuoanisha matukio ya kijabu na hali halisi, Dzombo anafunzwa mambo mengi akiwa huko *Walenisi*.

Baada ya kupitia hatua tofauti tofauti za kumbadilisha ili kujifahamu pamoja na kuelewa historia ya *Walenisi*, Dzombo anafunga safari kurudi alikotoka akiwa na mke (*Mtu-Mke Binti Fikinni*) ambaye anamwoa huko. Kwa hivyo ulimwengu huu mpya unakuwa kama funzo na kichocheo cha ubadilikaji wa Dzombo kama binadamu au kiumbe razini

Tunaweza kusema kuwa Walenisi ni nchi ya ajabu na hata matukio yake ni ya ajabu. Vivyo hivyo, utambuzi wake wa dhana ya wakati ni wa ajabu ukilinganishwa na wa Duniani, kwa mfano mwaka mmoja wa kiwalenisi ni sawa na miaka mitano ya kiduniani. Hata hivyo uajabu huo unaakisi hali halisi katika maisha ya ulimwengu.

Dhana ya wakati ni muhimu katika simulizi bunilizi kwa sababu matukio ya kibunilizi hutokea katika wakati na mahali maalumu. Tumeangazia dhana hii pamoja na njia mbalimbali inavyoweza kudhihinka katika riwaya ya *Walenisi*. Njia hizi ni pamoja na mpangilio, mtuo, udondoshi, idadi-marudio miongoni mwa nyingine.

Ni muhimu kukumbuka kuwa mifano iliyotolewa ili kuthibitisha njia hizo mbalimbali za kudhihinka kwa wakati sio yote. Kili cho muhimu ni kufafanua dhana fulani kikamilifu kisha kuitolea mifano. Hata hivyo tungetoa mifano yote kwa kila dhana ya kiwakati katika hadithi hii, bila shaka kazi hii ingekuwa ndefu sana.

SURA YA TANO

MPANGILIO NA UWASILISHAJI

Hadithi zinapowasilishwa huwa haziwasilishwi moja kwa moja. Waandishi aghalabu hutumia mitindo tofautitofauti katika uwasilishaji wa hadithi. Uegemezaji ni mojawapo ya mitindo inayotumiwa na waandishi ili kuwasilisha hadithi ambapo kuna hadithi ya kimsingi ambamo mna hadithi nyingine iliyoegemezwa kwa hiyo ya kimsingi.

Hadithi ya kimsingi ni ile hadithi ambayo inakuja kwanza (lakini sio kwamba ni hadithi kuu) ilhali hadithi egemezi ni ile inayofuata hadithi ya kimsingi, yaani inaegemezwa kwa hadithi ya kimsingi na aghalabu ndiyo hadithi kuu.

Kimsingi hadithi ya *Walenisi* imewasilishwa kwa misingi ya mtindo huu ambapo hadithi ya kimsingi inamhusu Dzombo tangu ahukumawe kifo kwa sayari hadi alipotua nchini Walenisi na yale yote yaliyompata akiwa njiani kuelekea huko

Hadithi **egemezi** ambayo imetegemezwa kwa hadithi ya kimsingi na ambayo inachukua sehemu **kubwa** ikilinganishwa na ile ya kimsingi ni ile inayosimulia kuhusu mwanzo wa Uchuna ambayo inafumbata visa vya moto, mchawi na mabavu. Kadhalika hadithi hii (egemezi) inagusia mfumo wa Uchuna na baadaye maanguko ya Uchuna

Hadithi egemezi katika nwaya hii ni changamano kwa jinsi ambavyo inahusisha hadithi nyingi zilizounganishwa pamoja ili kuchunguza na kuelezea historia ya nchi ya Walenisi. Mbali na kuelezea historia ya Walenisi, mwandishi aliegemeza hadithi hizi ili kutoa habari muhimu inayotoa picha mwafaka na kufafanua ni kwa nini Walenisi ilikuwa tofauti na Duniani alikotoka Dzombo.

Uwasilishaji wa aina hii ambapo pana hadithi ambazo zimepangwa pamoja kwa mfululizo unaofanana na ngazi una matatizo yake. Tatizo kubwa ni kwamba mtririko wake anaathirwa kwa kuwa mwandishi anatilia mkazo kwenye jambo analolisimulia

kuliko jinsi anavyoliwasilisha. Sababu yake ni kuwa katika uhakiki wa ki-naratolojia kama anavyosema Barry(1995:223):

*“kilicho muhimu si kile kinachowasilishwa
bali ni jinsi kinavyowasilishwa”*

Kadhalika tuanzapo kuisoma nwaya hii tunapatwa na msisimuko wa juu wa kutaka kuelewa yatakayotendeka pindi Dzombo anapoingia kwenye sayari hadi anapotua Walenisi ambapo kiwango cha taharuki ni kikubwa Lakini hali hii inabadilika Dzombo anapofika Walenisi ambapo kasi ya hadithi inapungua na kiwango chake cha taharuki kuathinwa, hali ambayo inatokana na mtindo wa usimulizi ambapo kuna matumizi mapana ya mbinu rejeshi na uegemezwaji wa hadithi

Tunakuta kwamba hali hii inabadilika hasa kutokana na kuwepo kwa visa ambavyo vina taharuki hasa vile vya waanzilishi wa Uchuna. Mwandishi anatumia visa hivi kama mbazi ya kukuza maudhui yake na vilevile kuchangia kiwango cha mvuto wa kisanaa wa nwaya hii.

Mpangilio wa aina hii (uegemezwaji) ni wa kimajanbio ambao unaweza kuathin usomekaji wa hadithi yenyewe kwa jinsi mwandishi alitumia idadi kubwa ya hadithi egemezi kwa hadithi ya kimsingi na hivyo hali hii inaweza kumtatiza msomaji kufuatilia mkondo wa hadithi

Ni muhimu kudokeza kwamba hadithi egemezi zinaweza kuainishwa katika aina tatu kuu(Barry 1995:227). Kwanza kuna hadithi egemezi ambayo baada ya kusimuliwa, msimulizi anarudia ile hadithi ya kimsingi. Kama tulivyoona hapo awali, hadithi ya kimsingi inamhusu Dzombo ilhali hadithi zilizoegemezwa ni zile zinazohusu mwanzo wa uchuna, yaani visa vitatu (cha moto, mchawi na mabavu), mfumo wa Uchuna na kuanguka kwa mfumo huo

Ili kuelewa uegemezwaji huu vema inahalisi kupanga muhtasari wa matukio yanayopakana katika nwaya hii kama ifuatavyo:

- a) Dzombo kushtakiwa
- b) Kupelekwa mahakamani.
- c) Kuhukumiwa kifo kwa sayari
- d) Kuingia sayarini
- e) Kupambana na majabali na kuyakwepa
- f) Kutua Walenisi.
- g) Kuanza sayari ya utu
- h) Kutaka kujua historia ya Walenisi.
 - Mwanzo wa Uchuna
 - Kisa cha moto
 - Kisa cha mchawi.
 - Kisa cha mabavu.
 - Mfumo wa Uchuna
 - Kuboromoka kwa Uchuna
- i) Dzombo kushawishika kujua historia ya Walenisi.
- j) Dzombo kumwoa Mtu-Binti Fikirini
- k) Dzombo kujiandaa kurudi nyumbani.

Matukio yaliyowasilishwa hapo juu kwa kutumia herufi ni sehemu ya hadithi ya kimsingi ilhali matukio yaliyowasilishwa kwa kutumia vistan ni hadithi egemezi, ambayo baada ya kusimuliwa, msimulizi anarejea kwa ile hadithi ya kimsingi. Yaani baada ya kusimulia jinsi Uchuna ulivyozuka na koo zake mbalimbali, hadithi kuhusu Dzombo (ya kimsingi) inarejelewa na tunaelezewa kuwa alimwoa Mtu-Binti Fikirini na kujiandaa kurudi naye *Duniani*.

Ni muhimu kukumbuka kuwa hadithi hii (ya kimsingi) inaporudiwa, inarudiwa katika muktadha tofauti ambapo Dzombo amepitia hatua mbalimbali za ubadilikaji na kuwa kiumbe mpya mwenye urazini. Mabadiliko ya utu wake na ya jamii kwa jumla (ikiwa

yatawezekana) yanaashiriwa na motifu ya safari yenyewe kuanza kutoka Duniani na pili katika safari mbalimbali alizozifanya akiwa Walenisi.

Athan mojawapo inayotokana na kurejelewa kwa hadithi ya kimsingi baada ya kusimuliwa kwa hadithi egemezi ni kuwa inachangia maudhui ya hadithi (nwaya) kwa jumla na hivyo kutoa ufafanuzi wa hali na miktadha fulani ambao unaweza kuwa umekosa katika hadithi ya kimsingi. Kwa mfano hadithi egemezi katika nwaya hii inafafanua ni kwa nini hali ya kimaisha iko jinsi ilivyo Duniani ikilinganishwa na Walenisi.

Aina ya pili ya hadithi egemezi ni penyezi, yaani hadithi egemezi ilio penyezi. Katika hali hii hadithi egemezi inaingiliwa au kukatizwa ili kurejelea hadithi ya kimsingi. Katika nwaya hii hadithi ya kimsingi inamhusu Dzombo na maisha ya Duniani lakini katika hadithi egemezi hasa ile ya sehemu ya mwisho inayosimulia jinsi Wachuna walivyounganisha mafiga tofauti ili kujiendeleza na kuanzisha utawala (Fyundusi) kuna upenyezi unaotukumbusha kuhusu Dzombo aliye kuini cha hadithi ya kimsingi. Katika ukurasa wa 195, tunasoma:

“Akimalizia mswada wake, Dzombo akasema ”

Hali hii inapotokea, inaonyesha mambo fulani kuhusu mtazamo wa hadithi. Kwa mfano hadithi hii egemezi katika nwaya hii inatolewa kwa nafsi ya kwanza, hata hivyo msimulizi anafika mahali na kujisahau na kubadili mtazamo na kuanza kusimulia kutoka kwa mtazamo wa mwandishi.

Vilevile, hadithi egemezi inapoingiliwa na msimulizi inamaanisha kuwa kuna udhaifu wa mtazamo unaotumika. Katika muktadha huu, mtazamo wa nafsi ya kwanza unaotumika kutoa matokeo ya utafiti una ufinyu kiasi fulani hasa pale kunahitajika kufuata wahusika fulani na kunpoti mambo fulani hasa kuhusu ndoto na sarkolojia zao. Kwa mfano katika ukurasa wa 192:

“akimalizia mswada wake, Dzombo akasema ”

ni usemi uliotolewa na mtu mwingine aliye nje ya hadithi inayosimuliwa kumaanisha kuwa mtazamo wa usimulizi umebadilika na kuwa wa nje.

Kadhalika, mwandishi hutumia hadithi egemezi penyezi kwa sababu za kimikakati kama vile kutenga msomaji kwa kuvunja ule mtiririko wa simulizi ili msomaji aweze kudadisi matukio fulani anaposoma. Kwa mfano mtiririko wa hadithi inayohusu uanzilishi wa koo mbalimbali unapovunjwa hasa katika sawia ya mtazamo, msomaji anajiuliza ni nani anasimulia. Ni Dzombo au ni mtu mwingine?

Aina ya mwisho ya hadithi egemezi ni ile baada ya kusimuliwa, msimulizi huwa harejelele ile hadithi ya kimsingi. Aina hii ya hadithi egemezi hapo katika hadithi ya *Walenisi*. Hata hivyo katika uhakiki wa ki-naratolojia wahakiki hushughulika na jinsi simulizi zimeundwa kwa kuonyesha ni vipi vipengee anuwai vya usimulizi vimedhihinka au kutodhihirika katika simulizi fulani.

Bila shaka, kazi za kifasahi huandikwa na mwandishi fulani ambaye anachukua nafsi ya mtu anayesimulia (msimulizi) hadithi hiyo. Msimulizi anaweza kujitokeza au asijitokeze waziwazi kama mhusika au asiwe mhusika. Kuna wakati mwingine ambapo mwandishi anajipenyeza (kama vile tumeona hapo juu) na kutoa maoni yake ili kutukumbusha au kutathimini jambo fulani.

Vile vile mwandishi anapopenyeza kwa kuingiza kauli fulani huwa anataka kupunguza au kurefusha masafa au umbali wa ujumi uliopo kati ya hadithi na msomaji ili aweze kupata picha kamili kuhusu matukio yanayosimuliwa.

Mbali na mpangilio wa hadithi, uhakiki wa kina-ratolojia unashughulika na namna ya uwasilishaji wa simulizi ambapo kuna jinsi au namna mbili kuu za uwasilishaji kama tulivyoona katika sura ya kwanza. Nazo ni mimesia na daigesia.

Mimesia hurejelea hali ya kuonyesha badala ya kusimulia (Wamitila 2003:127). Hivi ni kusema kuwa hadithi inawasilishwa kwa njia ya maonyesho katika mandhari mahususi

kwa kutumia dayolojia iliyojaa usemi halisi. Yaani kinachofanywa au kinachosemwa kinaigizwa kwa msomaji na hivyo kuzua hali ya kufikira kuwa anaona na kusikia, yaani angekuwepo angeona na angesikia.

Mkangi ametumia jinsi hii (mimesia) ya uwasilishaji si haba katika hadithi yake. Tunakumbana na dayolojia ya kwanza katika ukursa wa 6 ambapo kuna watu wanaotajwa kuwa ni wafadhaishwa. Katika mazungumzo yao, wanajiona kuwa wana bahati nzun ambayo mwenzao Dzombo hakuwa nayo na ndio sababu alihukumwa kifo.

Dayolojia inapotumika huwa inafupisha masafa ujumi baina ya msomaji na ulimwengu wa hadithi na kumfanya msomaji kuwa na hisia za huruma au chuki kwa baadhi ya wahusika kulingana matukio yanayojiri katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano Dzombo anapohukumwa kifo kwa sayari, mazungumzo yanayofuata (ya wafadhaishwa) yanazua hisia za huruma kwa Dzombo kwanza kwa sababu adabu yenyewe (kifo) ni kali na pili kwa sababu hakupewa fursa ya kujitetea kwa vile hakimu aliingia tu mahakamani na kutangaza hukumu ya kifo dhidi ya Dzombo.

Mazungumzo ya wafadhaishwa hao, vile vile yanazua hisia za chuki, yaani msomaji anawachukia wanavyomcheka Dzombo kwa kuhukumwa kifo kwa sababu inavyobainika baadaye ni kuwa Dzombo alipewa adabu ya kifo kwa kujanbu kuwahamasisha wanyonge (wakiwemo wafadhaishwa) kuhusu haki zao.

Ni muhimu kukumbusha kuwa, dayolojia hutokea katika hadithi hii baada ya msimulizi horomo (tazama sura ya pili) kusimulia na kisha kuwaacha wahusika wakizungumza wenyewe. Dayolojia imetumika katika hadithi nzima na popote inapotumika huwa inazua athari sawa kama ambavyo imetajwa hapo juu.

Mifano zaidi ya dayolojia iliyojaa usemi halisi ni pamoja na pale nduguye Dzombo anamweleza mwajiri wake kuwa angemnyonya (mwajiri) hali yake ingeimanka (uk 14-15). Pia kati ya Dzombo mwenyewe na mwajiri (uk 16-17), kati ya Dzombo ya karani wa kilimo (uk 19-21) pamoja na sehemu mbalimbali Dzombo akiwa Walenisi akizungumza

na wenyeji wake hadi alipomwoa Mtu-Binti Fiknni na kujiandaa kurejea Duniani. Tunaposema kuwa dayolojia imejaa usemi halisi inamaanisha kuwa kuna viwakilishi nafsi ya kwanza 'mimi' na 'ni' pamoja na alama za mtajo na kitenzi arifu. Kwa mfano katika ukurasa wa 20 kuna mazungumzo baina ya Dzombo na karani wa kilimo. Tunasoma:

"Acha kunitania!"

"Sio mzaha." akamwahakikishia.

"Mbona basi watufanya wajinga hivi?"

akauliza kwa hasira

"Sasa usin~~isumbue~~," karani akamwambia

"Nisikusumbue na ni nyinyi mlion~~ishauri~~

nilime mimea hii. . ." "Mimi siyaji hayo. - langu

ni ukarani tu." Akawa anajitoa lawamani

Katika dondoo hilo hapo juu, kiambishi 'ni' kimepigwiwa mstari popote kinapotokea. Kiambishi hicho pamoja na kiwakilishi nafsi 'mimi' ni ushahidi tosha kuwa ni usemi halisi. Kadhalika alama za mtajo na vitenzi arifu vinaonyesha kuwa maneno hayo yamenukuliwa jinsi yalivyotamkwa (tazama sura ya tatu). Ni muhimu kukumbusha kuwa dayolojia inapotumika haimaanishi kuwa mtazamo wa hadithi ni wa anayezungumza au wanaozungumza. Badala yake, mtazamo ni wa msimulizi wa nafsi ya tatu anayedokeza yanayoendelea kisha kuwaachilia wahusika wanaozungumziwa kuzungumza. Aina hii ya usimulizi kama tulivyoona katika sura ya pili inajulikana kama usimulizi horomo wa nafsi ya tatu.

Mbali na mimesia kuna namna nyingine ya kuwasilisha simulizi, nayo inajulikana kama daigesia ambapo usemi na matendo ya wahusika yanaelezwa na msimulizi (tazama sura 1). Hali hii inaakisi usimulizi maizi wa nafsi ya tatu kama tulivyoona katika sura ya pili. Katika hali hii msimulizi anaelekea kujua matendo yote ya wahusika, hisia na saikolojia zao.

Ni muhimu kudokeza kuwa hali hii (daigesia) ndio imetamalaki katika hadithi ya *Walenisi* ingawa mwandishi amebadili mitazamo ya hadithi hii kwa sababu za kimikakati, yaani pale mtazamo fulani hasa ule unaokwenda na usimulizi horomo unaoakisi uwasilishaji wa kimimesia unapotumika.

Ingawa mtindo huu wa daigesia umezoeleka kwa waandishi wengi, uhakiki wa kinaratolojia unapendekeza kuwa mimesia na daigesia zitumike kwa pamoja. Barry (1995:231) asema:

*"mchanganyiko wa mimesia na daigesia
hupelekea kuwa na hadithi ya urefu wa wastani"*

Hivi ndivyo Mkangi amefanya katika *Walenisi* ambapo kuna sehemu ambazo zimewasilishwa kwa njia ya dayolojia (mimesia) ambapo wahusika wanazungumza moja kwa moja kwa kutumia msemi halisi, na pia kuna sehemu ambazo zimewasilishwa kwa kutumia mtindo wa daigesia ambapo matendo na usemi wa wahusika yanaelezwa na msimulizi ambaye yuko nje ya ulimwengu wa hadithi na anayesimulia matukio ya hadithi jinsi anavyoyaona.

Hadithi hii inapoanza, mwandishi anawasilisha kwa mtindo wa daigesia ambapo tunaielezwa jinsi *Dzombo* anavyofikishwa mahakamani na kuhukumwa kifo kwa sayari bila kupewa fursa ya kujitetea. Punde tu baada ya sayari kufyatuliwa Mkangi anabadili mtindo wa uwasilishaji kutoka daigesia hadi mimesia ambapo anawasawiri baadhi ya watu wakizungumza kuhusu hali iliyomsibu *Dzombo* huku wakitoa maoni mbalimbali yaliyosheheni kinaya kuhusu hali ya *Dzombo* ambapo badala ya kumhurumia, walimcheka.

Mkangi anabadili kutoka daigesia hadi mimesia kwa sababu za kimikakati, yaani kutumia mitindo yote ya mimesia na daigesia kwa pamoja. Hivi ndivyo uhakiki wa kinaratolojia inavyo pendekeza.

Pia kubadili huku, kunatokana na sababu za kimtazamo ambapo mara nyingi mtazamo wa nje unaokwenda na daigesia unakuwa na mapendeleo kuliko mtazamo wa ndani.

unaokwenda na mimesia ambapo wahusika huzungumziana na kutoa maoni mbali mbali kuhusu tukio fulani.

Dzombo akiwa sayarini akitelekea mautini Mkangi anabadili tena kwa sababu tulizotaja hapo awali hadi mtindo wa daigesia na kumpitisha msimulizi maizi kusimulia jinsi Dzombo alivyopambana na majabali mbalimbali na kuyakwepa kwa ujasiri mkubwa na baadaye kutua nchini Walenisi. Tunasimuliwa kuwa alistajabia nchi hii kwa kiwango chake cha maendeleo na kuichukulia kama mbinguni.

Kama tulivyodokeza hapo awali kuwa uwasilishaji wa kidaigesia unakwenda pamoja na usimulizi maizi, basi msimulizi anamfuata Dzombo pamoja na wahusika wengine na kusimulia wanayofanya, wanayoyasema na kuyafikiria katika hadithi hii yaani popote wahusika wanasawiriwa kimaelezo (daigesia) bila wao kuzungumza ni mtindo wa daigesia uliotumika

Kimsingi sehemu ya hadithi ya *Walenisi* ambayo haijaakisi mtindo wa daigesia ni ile inayohusu utafiti wa Dzombo. Anapotoa taarifa ya matokeo ya utafiti wake, Dzombo anaeleza matokeo haya kwa nafsi ya kwanza yaani kwa mtazamo wake. Hata hivyo hali hii inabadilika na kuwa ya daigesia Dzombo anapoanza kuelezea (kutoka mtazamo wa mwandishi) kuhusu wachuna.

Kama tulivyoona hapo awali hali hii inatokea kutokana na ufinyu wa mtazamo unaotumika. Kwa mfano mtazamo wa kwanza (wa Dzombo) unashindwa kupenya akili za wachuna na kuonyesha fikira zao na hivyo kupelekea kubadilika kwa mtazamo.

Sehemu za simulizi ambazo zimewasilishwa kwa njia hii huwa zinawasilishwa kwa kasi na kwa muhtasari lengo lake ni kutoa taarifa muhimu kwa ufanisi zaidi, bila kujenga njozi kuwa matukio yanafanyika mbele ya wasomaji na hivyo kurefusha masafa ujumi kwa kusimulia kilichofanyika bila kuonyesha kilivyofanyika. Kwa mfano katika ukurasa wa 52 tunasoma

*"Kwa hivyo upinzani ulichukua muda mrefu
kuimarika kabla ya wao kutambua kwamba adu
wao alikuwa mmoja."*

Tunasimuliwa kuwa upinzani dhidi ya Uchuna ulichukua muda mrefu kuimarika lakini hatuoni jinsi Walenisi walivyofanya mikakati ya kuimarisha umoja wao dhidi ya wachuna badala yake tunasimuliwa tu. Hali hii inatoa maelezao ya matukio muhimu kwa muhtasari na hivyo kupelekea ploti ya hadithi kuwa na kasi zaidi.

Tulisema hapo awali kuwa uhakiki wa ki-nanatolojia unapendekeza kuwa uwasilishaji hadithi uchanganye mbinu za mimesia na daigesia. Hii ni kwa sababu hadithi iliyoandikwa kwa mtindo wa kimimesia pekee aghalabu huwa ndefu sana. Hadithi ya *Walenisi* ingeandikwa kwa mtindo wa kimimesia ambapo wahusika wangezungumza kutoka mwazo hadi mwisho ingekuwa na maelfu ya kurasa.

Fikina kuwa tungeonyeshwa mazungumzo yaliyojin mahakamani baina ya Dzombo na kiongozi wa mashtaka, mashahidi, kuairishwa na kurudiwa kwa kesi ya Dzombo hadi uamuzi kutolewa. Pia tuchukulie kuwa maelezo kuhusu wachuna na uchuna hayangekwepo, badala yake tuwe na mazungumzo ya wachuna katika shughuli zao za kila siku kwa miaka na miakaka ya utawala wao, basi hadithi ya *Walenisi* ingekuwa na urefu usiokadinka.

Vilevile hadithi ambayo imewasilishwa kwa mtindo wa kidaigesia pekee huwa fupi na inaweza kusomwa kama muhtasari wa ploti na inaweza kubana uhuru wa mwandishi kutumia baadhi ya mbinu za uandishi kama vile dayolojia ambayo inafumbatwa vema katika uwasilishaji wa kimimesia.

Hadithi ya *Walenisi* ingewasilishwa kwa mtindo wa daigesia pekee, basi bila shaka ingekuwa fupi sana. Lakini kwa vile mwandishi ametumia mitindo yote (mimesia na

daigesia) miwili, hadithi hii imekuwa na urefu wa wastani, yaani si fupi sana na si ndefu sana

Hata hivyo kuna wakati waandishi wanaweza kutumia mimesia na daigesia pamoja kwa namna kuwa msomaji asiye makini hawezi kuona kwa sababu mtindo mmoja unafumbata mwingine. Kwa mfano Dzombo anapotoa taarifa ya matokeo ya utafiti wake anafanya hivyo katika uwasilishaji wa kimimesia, lakini anapoendelea, mtindo unabadilika na kuwa wa daigesia ambapo Dzombo anatoa matokeo ya utafiti wake kwa kusimulia kama kwamba ni mtu tofauti, yaani anasimulia kutoka mtazamo wa mwandishi unaoakisi mtindo wa daigesia.

Tumeona kuwa tofauti ya kimsingi kati ya mimesia na daigesia ni kuwa katika mimesia tunaonyeshwa ilihali tunasimuliwa katika daigesia pasipo na kuonyeshwa. Hata hivyo katika daigesia msomaji anapaswa kuona yanayosimuliwa akilini mwake. Hivyo basi tofauti nyingine baina ya mimesia na daigesia ni mtazamo.

Uwasilishaji wa kimimesia unafumbata mtazamo wa ndani ambapo hadithi inasimuliwa katika nafsi ya kwanza. Hali hii inajitokeza katika ile schemu ya hadithi ambapo Dzombo anatoa taarifa ya utafiti wake. Hata hivyo bila kufahamu Dzombo anabadili mtindo huu na kutoa taarifa yake kwa mtazamo wa nje, yaani anaanza kusimulia juu ya Wachuna akiwa nje ya hadithi hivyo.

Sababu hasa ya kubadilisha mtazamo kama tulivyoona hapo awali ni kuwa mtazamo wa ndani (unaokwenda na mimesia) una upungufu wa kutoweza kupenya hadi akilini mwa wahusika na kuonyesha hisia na fikira zao za ndani kama mtazamo wa nje (unaokwenda na daigesia) unavyofanya

Katika sura ya pili, Dzombo anajisahau na kuacha usukani wa chombo cha mauti (sayari) na kuanza kufikiria ni vipi aliteswa akiwa mfanyikazi na vilevile akiwa mkulima. Katika hali hii Mkangi anatuonyesha matumizi ya mimesia na daigesia kwa pamoja hivi kwamba msomaji asiye makini hawezi kutambua

Kwanza kabisa, mwandishi anatumia mtindo wa daigesia kusimulia kwa kuonyesha Dzombo akiwa katika fikira akijanbu kuangazia yaliyomsibu kabla ya hukumu yake na hapo hapo tunaonyeshwa ni vipi alikuwa akizungumza na mwajiri wake na baadaye na karani wa kilimo Mazungumzo baina ya Dzombo na mwajiri wake na karani wa kilimo yanatokea akilini mwake na mwandishi amefaulu kuonyesha hayo mazungumzo kwa kutumia usimulizi maizi wenye sifa za kiungu za kupenya hadi akilini mwa Dzombo na kujua aliyokuwa akifikira.

Tunaweza kudai kuwa ile mifano inayoonyesha matumizi ya kisengerenyuma pia inaakisi hali ya kutumia mimesia na daigesia kwa pamoja. Dzombo akiwa Walenisi anakumbuka kisa cha Maskini Jeun na pia biashara haramu ya mzee Matigasi.

Mifano hii inaakisi mbinu rejeshi, kumaanisha kuwa mwandishi anasimulia kiulinganishi kuhusu Walenisi na Duniani. Lakini anapofanya hivyo anamsawiri Dzombo akiwa katika fikira nzito na kutuonyesha fikira hizo ambapo tunaona ni vipi anazungumza (Dzombo) na Maskini Jeun na vile vile ni vipi walevi walikuwa wakizungumza kuhusu mwanamke. Hali hii inaonyesha mimesia ndani ya daigesia yaani mitazamo miwili tofauti kwa pamoja kama tulivyoona katika sura ya pili.

Mbali na mifano hii ya mbinu rejeshi, hali hii pia inadhihirika katika ndoto zake Dzombo. Katika ukurasa wa 133-137 Dzombo anaota kuwa Binti-Fikiri amekuja katika chumba chake cha kulala na wanazungumza. Vilevile katika ndoto hii, Dzombo anamwona mkewe Hani na pia wanazungumza

Uwezekano wa kumsawiri mhusika katika ndoto upo ikiwa mwandishi atawasilisha sehemu ya ndoto kwa kutumia mbinu ya daigesia. Hivi ndivyo Mkangi amefanya kwa kutumia usimulizi maizi (wa nafsi ya tatu) na kupenya hadi akilini mwa Dzombo. Kadhalika katika ndoto hii, mwandishi amesawiri Dzombo akiwa katika mazungumzo na Mtu-Binti Fikirini ambaye alimwoa baadaye na vilevile na mkewe Hani huko Duniani.

Hali hii imewezekana kwa sababu mwandishi ametumia daigesia na mimesia kwa pamoja

Tumetilia mkazo mifano hii, ambapo mimesia na daigesia kama mbinu za kuwasilisha hadithi zimetumika kwa sababu ya upekee uliomo kwa mifano hiyo hivi kwamba inafumbata mitazamo miwili tofauti kwa pamoja. Hata hivyo tunaweza kusema kuwa hadithi ya *Walenisi* imewasilishwa kwa kutumia namna zote mbili za mimesia na daigesia na hatuwezi kutoa mifano yote ya kila moja ya namna hizi za uwasilishaji kwa sababu athari za kutumia mbinu hizi, kila moja katika upekee wake ni tofauti kama ambavyo imeonyeshwa. Kadhalika namna zote zikitumika kwa pamoja ni sawa, yaani kupelekea kuwa na hadithi ya urefu wa wastani. Kwa hivyo mimesia na daigesia huenda pamoja na aghalabu hufanya kazi pamoja na ni vipengee muhimu katika ujenzi wa simulizi

SURA YA SITA

6.0 HITIMISHO

Katika mtalaa huu, tumehakiki na kuinakidi nwaya ya *Walenisi* kwa kuzingatia kipengee cha usimulizi. Aidha tumeangalia vipengee anuwai vya usimulizi na kuonyesha jinsi vinavyodhihirika katika nwaya ya *Walenisi*.

Kipengee kimojawapo ambacho tumekishughulikia ni mtazamo na usimulizi ambapo tumeonyesha kuwa Mkangi ametumia mtazamo tofautitofauti kusimulia matukio katika hadithi hii. Sehemu kubwa ya nwaya hii imesimuliwa kwa mtazamo wa nje ambao kimsingi unatumia usimulizi wa nafsi ya tatu.

Kadhalika tumeonyesha ni vipi na ni kwa nini Mkangi anabadili kutoka mtazamo mmoja hadi mwingine kwa sababu za kimikakati. Kwa mfano, Mkangi anatumia mtazamo wa nje unaofumbata usimulizi maizi wa nafsi ya tatu ili kuwa katika hali nafuu ya kutusimulia matukio mbalimbali katika ulimwengu wa hadithi.

Kwa kufanya hivi, msimulizi wa nafsi ya tatu (maizi) anawafuata wahusika mbalimbali kila wanapokwenda na kusimulia matukio yote wanayoyafanya na hata kutuonyesha fikira, ndoto na saikolojia zao. Kwa mfano, akiwa sayarini kulekea kwa maangamizi msimulizi maizi wa nafsi ya tatu anampenya hadi akilini mwake na kuonyesha fikira za Dzombo ambazo zinategua kitendawili cha ni kwa nini alihukumiwa kifo.

Sehemu inayosimuliwa kwa nafsi ya kwanza inahusu utafiti wa Dzombo. Lakini kutokana na ufynyu wa mtazamo huu, Mkangi anabadili hadi mtazamo wa nje na kutumia usimulizi maizi wa nafsi ya tatu, ili kuweza kuwasawin vema wachuna na kuonyesha mienendo yao yote.

Pia tumeonyesha usimulizi horomo wa nafsi ya tatu unaokwenda na dayolojia. Hivi ni kusema kuwa, msimulizi horomo anasimulia na kisha kuwaacha wahusika wakiwa katika

mazungumzo. Hali hii inadhihirika katika riwaya popote kuna mazungumzo. Kwa mfano, baina ya wafadhaishwa na kati ya Dzombo na wahusika wengine katika riwaya

Vilevile tumejanbu kuonyesha mbinu za unenaji na fikra kama kipengee cha usimulizi. Mbinu za unenaji ambazo zinadhinka katika riwaya ni nne. Kwanza kabisa kuna usemi halisi ambapo maneno yananukuliwa moja kwa moja kama yalivyotamkwa na mnenaji ambapo kuna matumizi ya alama za mtajo na viwakilishi nafsi ya kwanza

Mbinu nyingine ya unenaji ni usemi wa taarifa ambapo maneno yaliyosemwa na mtu mwingine yanapotwiwa. Hali hii inadhihirika njeo ya wakati uliopita inapotumika pamoja na kuondolewa kwa sifa za usemi halisi kama vile alama za mtajo na viwakilishi nafsi ya kwanza na badala yake kutumika kiwakilishi nafsi ya tatu 'a' katika umoja na 'wa' katika wingi.

Mkangi, vilevile ametumia mbinu nyingine za unenaji. Hizi ni pamoja mfumo ulio wazi zaidi kuliko usemi halisi na mfumo mwingine ulio funge zaidi kuliko usemi wa taarifa. Mifumo hii yote tumeiangalia na kuonyesha jinsi inavyodhihinka katika riwaya hii. Kipengee kingine ambacho kimeshughuliwa kwa mapana ni kipengee cha wakati na ni vipi kimedhihinka katika hadithi ya *Walenisi*. Tumeonyesha vigezo muhimu vya kushughulikiwa tunapojadili suala la wakati katika hadithi. Vipengee hivi vya wakati ni pamoja na mpangilio, muda, idadi-marudio miongoni mwa vingine. Vipengee hivi vimejadiliwa na kutolewa mifano ainati ya kuonyesha kudhihinka kwao.

Mwisho kabisa tumeshughulikia kipengee cha mpangilio na uwasilishaji wa simulizi. Katika muktadha huu tumeonyesha ni vipi hadithi ya *Walenisi* ina hadithi ya kimsingi inayomhusu Dzombo na hadithi nyingine egemezi zilizoegemezwa kwa hadithi ya kimsingi

Kadhalika tumeonyesha aina za hadithi egemezi na athari zake katika *Walenisi*. Aidha tumeshughulikia gamna au jinsi ya uwasilishaji wa hadithi ya *Walenisi* ambapo tumeonyesha kuwa kuna namna mbili za kuwasilisha simulizi. Njia hizi ni mimesia na

daigesia ambapo tumejadili maana na athari za matumizi ya mbinu hizi na kisha kuonyesha kudhihirika kwao katika riwaya hii.

Kimsingi, tunaweza kusema kuwa tumeonyesha kudhihirika kwa vipengee anuwai vya usimulizi katika riwaya ya hii. Hivyo ndivyo uhakiki wa ki-naratolojia unavyohitaji kwa sababu kilicho muhimu si usomaji na ufasiri wa hadithi yenyewe, bali ni jinsi hadithi imeundwa kwa kuzingatia vipengee mbalimbali vya usimulizi.

6.1 MATOKEO

Katika utafiti wetu, tumegundua kuwa usimulizi ni mpana kiasi kwamba haiwezekani kuushughulikia ipasavyo katika tasnifu hii. Vile vile tumegundua kuwa hadithi ya *Walenisi* imefumbata kwa kiasi kikubwa baadhi ya vipengee vya usimulizi kwa mitarafu ya Genette ambaye tulitumia mawazo yake katika utafiti huu.

Hata hivyo, tulipoangalia mpangilio na uwasilishaji kama kipengee kimojawapo cha usimulizi, tuligundua kuwa aina mojawapo ya hadithi egemezi haidhihiriki katika hadithi ya *Walenisi*. Katika uianishaji wa hadithi egemezi, tuligundua kuwa, ile hadithi egemezi ambapo hadithi egemezi hairejelewi baada ya kusimuliwa kwa hadithi ya kimsingi ndiyo haipo katika *Walenisi* na hivyo kukisia kwetu katika hypothesis kuwa muundo wa hadithi ya *Walenisi* umefumbata vipengee vyote vya usimulizi kutoafikiwa.

Kadhalika, tuligundua kuwa ingekuwa vema kushughulikia kipengee kimoja tu katika usimulizi badala ya ya kutamba katika vipengee mbalimbali. Tulipogundua hivi, tayari tulikuwa tumepiga hatua katika utafiti na ikawa vigumu kubadilisha mada ya utafiti. Tulipendekeza, katika sura ya kwanza kuwa tungesoma riwaya nyinginezo za Mkangi, ili kupata mwao kuhusu mtindo wa uandishi wake na tuligundua kuwa mtindo wa usimulizi katika *Walenisi* unafanana na ule wa riwaya ya *Mafuta*. Mbali na kufumbata vipengee vingine vya usimulizi, Mkangi ametumia uegemezaji katika riwaya hizo mbili kwa sababu za kimikakati, kama tulivyoona hapo awali katika sura ya tano.

Tumeclezea kwa uwazi katika sura ya kwanza kuwa, tuliongozwa na nadhana ya naratolojia katika utafiti wetu ambapo tuligundua kuwa nadhana yenyewe ina udharifu. Kwa mfano, kwa nini tushughulike na fikra ambazo ni yaliyomo (maudhui) ilhali nadhana inapendekeza kuwa inashughulika na miundo ya simulizi? Hapa tulipata kuwa nadhana yenyewe inajipinga

Kadhalika tuligundua kuwa hadithi ya *Walenisi* ina muundo changamano kwa jinsi ambovyo imetumia uegemezaji kwa kiasi kikubwa, na hivyo kuafikiana na kukisia kwetu katika mojawapo ya hypothesis zetu

Katika utafiti wote kunatokea na matatizo ya hapa na pale. Baadhi ya matatizo hayo ni kama vile ni ukosefu wa vitabu katika maktaba yetu, ambapo tulikuta kwamba vitabu havipo na ikiwa vipo, basi ni vichache au ni vile vya zamani ambavyo mawazo yao yamepitwa na wakati na vinahitaji kuandikwa upya

6.2 MAPENDEKEZO

Baada ya tafiti huu tungependekeza kuwa usimulizi ni mpana hivi kwamba tuliyafanya ni machache kuhusu dhana hii na wasomi wa fasihi ya Kiswahili wanaweza kushughulikia vipengee vya usimulizi kwa kina zaidi.

Kwa vile utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya naratolojia, tungependekeza kuwa wasomi wengine wanaweza kuhakiki riwaya hii kwa kutumia nadharia nyingine kama vile umuundo ili ni kuchanganua muundo wa riwaya hii kwa kina zaidi

Katika utafiti wetu, tumehakiki *Walenisi* kwa kuzingatia kipengee cha usimulizi kwa kijumla kwa kuvitongoa vipengee unuwar vya usimulizi na kuona ni vipi vinadhahika katika kazi hii. Kwa hivyo, tungependa kutoa changamoto kwa wasomi wa fasihi ya Kiswahili kuvishughulikia vipengee vya usimulizi kwa kina zaidi

Kadhalika tungetoa changamoto kwa wananadharia katika fasihi kuwa nadhana ya natolojia inajipinga na hivyo ifasiliwe vema ili kubaini teneti zake kwa uwazi zaidi.

MAREJELEO

- Aligula R.E.(2003): *Mwongozo wa Walemsi*, Eldoret, Bookshelf Publishers
- Barry P.(1995): *Begining Theory*, New York, Manchester University Press
- Booth C W (1961): *The Rhetoric of Fiction*, Chicago University Press
- Chatman. S. (1990): *Coming to terms: the Rhetoric of Narrative in Fiction and Film*, Ithaca Cornell University Press
- _____ (1978): *Story and Discourse: Narrative Structure in Fiction Film*, London, Cornell University Press.
- Culler J(1975): *Structuralist Poetics: Structuralism, Linguistics And The Study of Literature*. New York Cornell University Press
- Foster E M(1927): *Aspects of The Novel*, London, Penguin Books.
- Genette, G (1980): *Narrative Discourse: An Essay in Method* Ithaca, Cornell University Press.
- Geoffrey N.L. & Michael H.S. (1981): *Style in Fection: An Introduction to English Fictional Prose*, Longman Inc. New York
- Harvey, J W(1965): *Character And The Novel*, London Chatto and Windus Ltd

- Hornbe A S (1948): *Oxford Advanced Learners Dictionary*,
OUP New York
- Hough, G (1962): *An Essay in Criticism*, London Gerard Duckworth
and Co. Ltd
- Katama, G M (1995): *Walenisi*, Nairobi, EAEP
- _____ (1984): *Mafuta*, Nairobi, Heinman Educational Books
- _____ (1975): *Ukiwa*, Nairobi, Oxford University Press
- Leberman, M M &
Foster E E (1968): *A modern Lexicon of Literary Terms*
Atlanta USA, Foresman Lothe & Co
- Lothe J ,(2000): *Narrative in Fiction and film: An Introduction*,
New York OUP
- Mieke Bal (1985): *Narratology*, Toronto, Toronto University Press
- Mohamed, S A (1995): *Kunga za Nathari ya Kiswahili*, Nairobi EAEP
- Njogu K and Chimerah (1999): *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu*.
Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation
- Philip G G (Ed) (1976): *Websters Internatonal Dictionary*,
G&C Marrian Co.
- Propp, V (1968): *Morphology of The Folktale*, Austin, University
of Texas Press.

- Richard, G (1995): *Mastering English Literature*, London, Macmillan Press Ltd.
- Rimon-Kenan S. (1983): *Narrative in Fiction: Contemporary Poetics*, London Rout Ledge.
- Scholes, R & Robert K (1966): *The Nature of the Narrative*, London, OUP
- TUKI(2000): *English-swahili Dictionary*, Dar es Salaam Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- _____ (1981): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* Dar es Salaam. OUP
- Wamitila K W (2003): *Mwongozo wa Walenisi* Nairobi, Sasa Sema Publications.
- _____ (2003): *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Nairobi, Focus publications Ltd.
- _____ (2002): *Uhakiki wa Fasihi: Misingi Na Vipengele Vyake*, Nairobi, Phonix publishers (k) Ltd.
- Wasike, M (2003): *Mwongozo wa Walenisi* Nairobi, Avenue Publications Ltd